# Pambazuko

Toleo Nambari 20180198334 | Septemba 18- 24, 2019 | Gazeti Lako Rasmi | Ksh 40


UK 20- 21




# KIBRA: MARIGA NI MKUKI MOYONI MWA ODM



**“Wahenga walisema siri ya mtu ni jipu la moyo na uamuzi wa IEBC kumruhusu McDonald Mariga kushiriki kuwania uchaguzi mdogo wa Kibra, utawafanya wapinzani wake kuweweseka kila usiku uchao.”**
Uk 4

## JUMWA ASUTWA KWA KUMWITA KEN CHONGA KIKARAGOSI



NA ALFRED KITI

Mbunge wa Malindi Aisha Jumwa amekashifiwa vikali katika mitandao ya kijamii ya makundi ya jamii ya wachonyi ambao ndio wengi katika eneo bunge la Kilifi Kusini baada ya kutoa matamshi ya matusi dhidi

Inaendelea UK 5 >>>




“Kijana mmoja awalilia Waree wamurai babake ili amregeshee bibi yake ambaye aliinyang’anywa na mzazi wake aliyeamua kumchota mkaza mwanawe.”
Uk 10

## ADAI HAKI BAADA YA BABAKE MZAZI KUMNYANG’ANYA MKEWE

https://t.me/magazeti


Don’t miss your Saturday and Tuesday Standard to learn from the past

For ALL the 2019 KCPE and KCSE Candidates!

Tutor-Soma Tu
PAST PAPER REVISION SERIES

# Kasumba ya leo imeondoa uadilifu, heshima na nidhamu katika maisha

Mswahili limemshtua sana na kukumbuka zama za ujana wao wakiwa watoto, wakawa mabarobaro. Vijana ambao leo wamekuwa wazee na mambo mengi kuyaona na kupitia. Siyo mabaya wala mazuri yote wameshuhudia na maisha yanaendelea ijapo wanajipa funzo la maisha.

Ndio hali, kila palipo na wazuri wabaya hawakosekani, ila wabaya hao wa wakati ule, walifanya maovu kwa kujificha sana, kwa haya nyingi na uwoga. Walikuwa wakitoka hasa na kuenda kuyafanyia maovu yao mbali na kwao.

Zamani hizo, wabaya wakigunduliwa, hutengwa na jamii na mara nyingi walifukuzwa wagurie miji mingine. Kila jamii iliogopa sana kuaibika, au kuingia dosazi mbele za jamii nyingine.

Kwahiyo waliyaangalia kwa makini mienendo ya vijana wao na kuifuatilia kwa karibu sana, nidhamu, mila, desturi na taratibu zote za ukoo wao. Haikuwa rahisi kutekeleza hayo, Ila jamii ilijipanga kwa kufuata marika yalio wagawa kwa makundi. Vijana waliwekwa kwa kundi lao, watu wazima na wazee makundi yao na huku kuna watoto na akina mama. Kwa ujumla waliheshimiana na kuaminiana kwa kila kundi kujua wajibu wake katika jamii.

Wazee walikuwa ndio wapatanishi na wenye kufuatilia masuala mazito kama vile magonjwa ya mlipuko, ukame na vita. Maamuzi yao au ushauri wao ulikubaliwa na kufatwa pasipo maswali ya kijinga kama tulivyo hali hii ya leo.

Mswahili awaza sana na kushangazwa juu ya haya yaliojitokeza na kuwa donda ndugu lisokuwa na dawa. Anajiuliza ni kasumba ipi iliyo tuingia kiasi kwamba tumekosa uadilifu, heshima na nidhamu ya maisha.

Hivi mtoto wa kike, bado msichana mwana mwali, anasaoma ni rika na binti wako au mdogo kuliko binti wako, wamrubuni na kutembea naye kimapenzi, bila kuona haya wala roho kukusuta.

Wampa uja uzito, wamuharibia masomo na maisha yake, anakuwa mzigo kwa Taifa. Ni wapi tunapo kosea? Je ni laana au ndio mwisho wa Dunia? Yasemekana humu nchini mwetu, asilimia hamsini ya watoto wanao zaliwa, ni wa nje ya ndoa. Na asilimia ishirini na tano ni watoto wa mzazi mmoja, yaani watoto wa mama wakilelewa na mama pekee.

### Watumaarufu

Watoto hao wanakosa haki zao za msingi toka kwa baba zao ambao wengine ni watu wakubwa ambao wana nyadhifa na matajiri. Wamewatelekeza na kuwachia mama zao kuwalea au kuwaacha wawe watoto wa mitaani ama hayawani.

Hawapati mahitaji muhimu na wala hawapati mapenzi ya kulelewa kama wenziwao wanao lelewa ni wazazi wao wote. Hawapati huruma za wazazi wao, ila wanakuwa wakiwa wapweke, yatima wanasonono moyoni na usongo wa mawazo yasio na hatima.

Mwisho wa fikra na matamanio na hamu ya kuwa kama wenziwao wanapoyakini kuwa hawaipati tena wanageuka na kuwa makatili wasio haruma, wanaweza kufanya lolote wakati wowote bila kujali huyu ni mama au baba. Roho zao zimeshaingia kutu, zimesinyaa zimekatatamaa.

Chanzo cha yote hayo ni ngono zembe, ngono zenye kuwadhulumu haki wasichana wadogo kwa kuwarubuni kwa pesa na vitu vya tunu. Tunajenga taifa la kesho la watu wa aina hiyo. Tunategemea kutakuwaje? Usisahau na wewe unayefanya hayo, wanao pia watafanyiwa hayohayo.

Kutokana na utafti huo, imedhiri kwamba miji mikubwa inaongoza kwa mimba za utotoni, kuka na kunajisiana. Huku ndiko kwenye ustaarabu unaoigwa na wengi ukapelekwa bara.

Leo ndio kumekuwa na lawama hizo za matendo ya kinyume na ustaarabu wa asili wa mswahili mwenye maadili mila desturi na tamaduni ilio bora. Mswahili anauliza, Ni nini kimewakumba waungwana hawa? Mwataka kujenga vizazi vijavyo vya aina gani? Watoto hawa watajinasibu vipi ikiwa hawazijui nasaba zao?

Hamuoni watatukanwa kudharauliwa na kunyanyasika kila wanapo kuwa mbele za wenzao walio lelewa na wazazi wao walikuwa kwenye ndoa? Hamumuogopi hata Mungu anae kataza zinaa?

Yaani zinaa mnaifanya mapambo kwenye jamii? Kwa hali hiyo ilivyo ndio tuseme kwa wastani kila nyumba huku kuna mtoto wa nje ya ndoa? Inna lilah wainna ilayhi rajiuun, Msiba mkubwa.

### Usipoziba ufaa

Inasikitisha mno, ina kera inatia uchungu, hasa kuona kaunti zetu ndio zinammomonyoko wa maadili. Haipendezi wala si sifa bali ni kashifa. Vyema tutafute njia ya kuliziba hili, kabla halijakuwa la kujengewa ukuta.

Napenda niwarudishe nyuma sana tu, mwanzoni mwa Gazeti hili kuzinduliwa, nilizungumza juu ya, mila na desturi za waswahili hususan wa pwani katika kuwalea watoto wao.

Walitumia jando na unyago kuwa njia ya kuwasomesha watoto wao Malimwengu walimwengu na Ulimwengu. Wakitoka jandoni na unyagoni, vijana hua wamejua hatari za ngono zembe. Msichana anajijua yeye ni shamba ikipandwa mbegu itamea. Alijitahadhari, akajiepusha na mapenzi, akawa hodari wa kukwepa vishawishi, mimba za utotoni zilikuwa hapa mno, moja kwa mia.

Mswahili natoa rai yangu katika kupambana na hili janga, sisemi lifatwe bali liangaliwe kwa undani kisha mulijadili kwa kina. Ni vyema tuweke zawadi kwa wasichana watakao maliza shule wakiwa bikira, zawadi nono tu huenda ikapunguza wimbi hili la mimba wakiwa shulemi.

Pili watakaowapa uja uzito wanafunzi watafutiwe adhabu kali zaidi ya kutisha. Tusiwaonee haya wasiokua na haya kwa wasichana wetu. Maana waswahili wanasema kata pua uunge wajihi.

Tatu wazazi wasibague, wamuona msichana anarubuniwa watazama tu na kusifia, eti jamaa ana kasichana kadogo. Huo ni ujinga ndugu yangu, mkemee yule mwanaume na mfokee msichana umuonye kwa hasira ili asirudie.

Wazazi wote tuwachukulie wasichana wote ni wetu sisi sote. Tuwe pamoja kuwalinda. Na yule atakae kuwa hataki atengwe na aondolewe kwenye mtaa wenu. Ni kuamua kupigana vita vya maneno ya kukanyana, bila kuogopana kwa visingizio eti mwajuana. Kujuana kwa kuharibiana, bora musijuane.

Mswahili anajua anawachoma wengi, lakini huwezi kufunulia shonde kwa shuka nyeupe ukidhani umeepuka izara, harufu itakuumbua.

Tayari yaliokuwa yameshakuwa, tujitahidi yajayo yasiwe. Mpende mtoto wa mwenzio kama unavyo mpenda wako. Nakutahadharisha na kukumbusha kwamba, usihadaike na uzuri na mapambo ya bucha nyama ni ileile tu.

Ladha na utamu wa chochote ni hisia zako wewe mwenyewe. Hakuna jipya ulisikialo unapo badili badili zaidi ya kujitia kwenye hatari ya kuoata maambukizi.

Mswahili bwana! Donge kalicheua, wanao kereka wakereke, Ila haliwi zito kwa mja mwelewa. Tafakari.



## VISA VYA MITAANI

Na Juma Mrisho

# Ni ukweli wa machungu mama apewa na mtoto juu ya babake


Baba mmoja mkosa adabu, alikuwa na dada wa kazi chumbani wakila uroda. Mara mtoto wake wa kiume wa miaka mine akaingia ghafla akawakuta, maana alisikia kelele. Aliuliza bila kujua kinacho fanyika, Baba mbona dada wakazi analia, unampiga?

Baba akajibu haraka, “Hapana nampakaa dawa”.

Mtoto akatoka, siku zikapita, siku nyingine akasikia makalele mamake akilia akaja mbio akasukuma mlango akawakuta habari ndio hiyo ya moja kwa moja wanahabari siku hizi wakaipachika “live”.

Mtoto akasema “Mama hata dada wa kazi alikuwa anapiga kelele, lakini alipona. Dawa hiyo inaumaaaa!

Mimi sijui ilikuwaje baada ya mama mwenye nyumba kujua kumbe dada wa kazi pia hupewa dawa.




https://t.me/magazeti

# Aponyokwa na kikoi mbele ya babamkwe, mashemeji

Kijana wa bara ambaye ameishi kiasi pwani na akabahatika kuoa, akaamua kwenda ukweni kuwatembelea.

Walikaribishwa, babamkwe akamwita msichana wake ambaye ni shemeji wa kijana kwenda kuangua dafu.

Kijana akaona si heshima, akaamua aende yeye. Nikukumbushe tu kijana naye kavaa kipwani mavazi ya kikoi singi lendi na kanzu. Kijana akavua kanzu akabaki na kikoi na singi lendi, wakaongozana na wakeze pamoja na shemeji zake wawili na mkewe.

Na kweli ajua kupanda mnazi, akapanda vizuri kafika juu kasahau kisu. Ikabidi shemeji asogee chini ya mnazi amrushie, akitupa jicho juu aona dafu mbili zikining’inia.

Shemegi hakusema kitu alijikaza kucheka ila akamrushia kisu akakidaka, kumbe awatikisa mayavuyavu ama siafu wa mnazini.

Siafu wakaja wakamuuma akaachia mnazi, akaanguka kile kikoi kikamuacha kama alivyozaliwa!

Baba mkwe akawaambia bintizake; “Shemeje yenu huyo, msitirini, mkewe amchukue na kumfunika shuka”.

# Trump amfuta mshauri wake, 10 kuwania urais



Rais Donald Trump na mshauri wake aliyemtimua John Bolton

**WASHINGTON DC:**

Donald Trump rais wa sarakasi na vituko wa Marekani amewashangaza walimwengu tena kwa kumfuta mshauri wake mkuu wa usalama John Bolton.

Katika taarifa yake fupi Trump asema hakuweza kukubaliana na Bolton katika maswala nyeti aliyopendekeza kwake.

Wadau wakiwemo wachanganuzi wa kimataifa wa kisiasa wanamini kuwa Bolton alikuwa na msimamo mkali wa kivita na aliweza kumtumia Trump katika falsafa hiyo hatari.

Yasemekana Bolton alitaka Marekani iwe na msimamo mkali dhidi ya iran na hata kuishambulia lakini Trump alisita.

Mshauri huyo mwenye nyusi na ndevu nyeupe kama paka mwanga asemekana alichukia uislamu sana lakini kuenzi na kupendelea taifa la kiyahudi la Israeli.

Akipongeza hatua hiyo ya Trump kiongozi mkuu wa Iran Hassan Rouhani alisema ni habari nyeti na ya kutia moyo kwa Marekani kujitenga na watu wanaochochea vita dhidi yake na mataifa mengine.

Hatahivyo Rouhani anasisitza kuwa kufutwa kwa Bolton si kigezo cha kubadili uamuzi wake wa kutokutana na Trump mpaka vikwazo vyote dhidi ya Iran vitakapoondolewa bila masharti yoyote.

**10 wataka tikiti kumpinga**

Kundi la wapiganiaji 10 wanakamia tikiti ya chama pinzani cha Democratic ili kumshinda Donald Trump katika uchaguzi wa mwaka ujao.

Trump wa chama tawala cha Republican anangoja mshindani wa Democratic kwa kinyang'anyiro hicho bab kubwa.

Trump amelaumiwa kwa siasa mbovu katika maswala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.Wengi wanamuona mtu m'baguzi asiyetaka wageni kwa sera zake kali za uhamiaji.

Mbinu za kiuchumi za Trump zimelaumiwa kwani amekata mahusiano ya mshirika wake mkuu wa kibiashara China kwa wivu wakushindwa na mabwana hao wa macho madogo lakini akili kubwa kama kunguni.

Je, nani atakuwa mpinzani wa kufaa wa kumshinda Trump safari hii? Wadadisi wanamini kuwa wagombeaji wawili kati yahao 10 wana nafasi kubwa ya kutua White House na kumfurusha Trump.

Wawili hawa ni aliyekuwa makamu wa Rais wa Barrack Obama yaani John Biden wa umri wamiaka 76 na mzee mwenzake Bernie Sanders wa miaka 77.

Hatahivyo wawili hawa lazima kwanza wapate tikiti kwa kuwabwaga wenzao.Baadhi ya hawani kina mama Kamal Haris, Army Klobuchar na Tulsi Gabard.

https://t.me/magazeti



## Waandamana dhidi ya ubakaji Afrika Kusini

**PRETORIA**

Maelfu ya waandamanaji walimiminika barabarani kushutumu kukithiri kwa ubakaji kiholela dhidi ya wanawake nchini Afrika Kusini.

Utafiti unaonyesha kuwa kwa kila nusu saa ama sekunde kama 36 mwanamke ama kisichana kimoja hubakwa katika nchi hii ilojaa uhalifu wa kila aina.

Katika miji ya Afrika Kusini kama Pretoria , Cape Town na haswa Johanesburg ubakaji au unajisi ni jambo la kawaida.

Hali hii imefanya mashirika ya haki za binadamu na watetezi wa jinsia ya kike kujitokeza na kulaani tabia hii mbovu.

Afrika kusini ndio nchi inayongoza kwa maambukizi ya gonjwa hatari la ukimwi.Yamkini ubaka.JI ndio moja ya sababu kuu ya kuenea kwa ukimwi nchini humo.

## Kimbunga cha Hurricane chavamia kisiwa cha Bahamas



**BAHAMAS:**

Kimbunga hatari kutoka bahari kuu ya Atlantiki kinachokwenda kwa kasi ya ajabu kimeleta maafa makubwa kisiwani Bahamas.

Kimbunga hicho kinachojulikana kama Huricane Dorian huzunguka kwa mviringo baharini kwa kasi ya takribani kilomita 300 kwa saa.

Nchini Bahamas katika pwani magari na nyumba sambamba na miundo mbinu ziliangamizwa na kimbunga hichi hatari.

Yasemekana watu 50 wamepoteza maisha, mali kuharibiwa na watu 1,300 hawajulikani walipo mpaka sasa.

Serikali ya Marekani imeahidi kutowa mamilioni ya dola kuwasaidia wabahamas.

# Tofauti kati ya familia ya Mugabe na Rais Mnangagwa kuhusu mipango ya mazishi

**HARARE:**

Hatimaye familia ya marehemu Mwenda zake na baba wa kwanza wa taifa wa Zimbabwe, Robert Mugabe wamedhihirisha uchungu wao kwa serikali ya Rais Emmerson Mnangagwa kwa kutofautiana mipango ya mazishi.

Robert Mugabe atazikwa nyumbani kwao kjijiji cha Kutama baada ya familia yake kukataa mpango wa serikali kumzika kitaifa na kishujaa jijini Harare.

'Hatutaki unafiki. Wakati walipompinduwa Mzee walifikiria nini? Mzee hana radhi nao na kwani wana haki gani kupanga mazishi bila ushauri wetu?' alisema mmoja wa jamaa wa Mugabe.

Familia ya Mugabe ilichukizwa na serikali hiyo ya Rais Emmerson Mganangwa aliyesaidiwa na majeshi kumpindua Mugabe kuandaa mazishi hayo.

Viongozi mbali mbali walihudhuria mazishi hayo yaliyofanyika kilomita takribani 90 kutoka Harare.



Rais Emmerson Mnanangawa akishauriana na Grace Mugabe walipoipokea mwili wake Robert Mugabe mjini Harare, Zimbabwe.

# KIBRA: MARIGA NI MKUKI MKALI MOYONI MWA ODM

**"Wahenga walisema siri ya mtu ni jipu la moyo na uamuzi wa IEBC kumruhusu Mcdonald Mariga kuwania uchaguzi mdogo wa kiti cha ubunge cha Kibra, utawafanya wapinzani wake kuweweseka kila usiku uchao."**



Mgombea wa kiti cha Ubunge cha Kibra kwa tikiti ya ODM Imran Okoth.

https://t.me/magazeti

**NA RIPOTA WETU**

Wadadisi wengine wa siasa, wameichukulia ODM sawa na timu ya Uingereza ya Arsenal ambayo pia ndiyo kipenzi cha kinara Raila Odinga na msururu wa wanachama chungu nzima hapa nchini. Sawa na Arsenal, ODM pia huanza kampeini zake na kufululiza kwa mbwembwe nyingi lakini hatimaye, huishia ngamani na kuwavunja mioyo wengi wasijue wapi wameenda kombo.

Taarifa kwamba tume ya uchaguzi nchini ya IEBC imemwidhinisha rasmi mwanasoka Mcdonald Mariga kuwania uchaguzi mdogo wa Kibra wa Novemba 7, imelazimu usimamizi wa kampeini ya mgombea wa tikiti ya ODM Imrani Okoth kufungua ukurasa wa mbinu mpya.

Awali, viongozi wa ODM wakiongozwa na kinara Raila Odinga, walikuwa na afueni ya kukabilina na wagombeaji wengine mswaki kabisa kutokana kwamba wagombeaji hao katu hawababaishi wala kuzuia kimbunga cha saisa chama hiki.

### Hatua ya Raila

Punde habari zilipotapakaa kwamba mgombea wa Jubilee ameruhusiwa kuendeleza kampeini zake, usimamizi wa ODM uliamuriwa mara moja na kinara wake kuhakikisha kwamba wagombeaji wote walioshindwa kwenye mchujo waitwe mara moja na kuregeshewa pesa zao.

Hatua ya kinara wa upinzani na chama cha ODM Raila Odinga ya kuwaregeshea pesa wagombeaji walioshindwa kwenye mchujo wa uchaguzi mdogo wa Kibra, ni dalili kamili kwamba kuchipuka upya kwa Mcdonald Mariga wa Jubilee ni tisho linalohitaji umoja chamani.

Hii ni baada ya kugundua kwamba usimamizi wa chama uliosimamia mchujo wa ODM ulighafulika kwa kutotii kanuni za chama kwa kuwepo njama fiche kati ya maafisa wakuu fulani wa chama kuhusiana na orodha kamili ya uanachama wa ODM eneo bunge la Kibra.

Baada ya kuona dosari hilo, kinara wa chama Raila Odinga ameonelea kuwarai wagombeaji wote walioshindwa mchujoni kwa kumregeshea takribani shilingi 250,000 walizotoa kama ada ya chama ya kuwania wadhifa huo. Raila aliregeshea wagombeaji hao jumla ya shilingi 2.5 milion.

Waliopokea malipo yao ni pamoja na Mwalimu Mkuu wa shule ya upili ya Dagoreti High, Peter Orero ambaye asemekana ndiye aliyekuwa maarufu zaidi ya wote kwa upande wa ODM. Wengine ni Ben Musungu, John Otieno, Chris Odhiambo na Tony Ogola miongoni mwa wengi.



Mwanasiasa wa Jubilee McDonald Mariga akabithiwa cheti na ofisa wa uchaguzi wa IEBC Beatrice Muli. Uchaguzi mdogo wa Kibra utafanyika mnamo Novemba 7.

### Umoja ninguvu

Uongozi wa ODM yaaminika utakosa usingizi siku chache zijazo ili kuzama na kuzuka kuja na mbinu za kukabilia Mariga ambaye kwao wanamuona moja kwa moja kama mbuzi inayolisha Kibra ikiwa na kamba shingoni inayoshikiliwa na Naibu Rais William Ruto.

Kwa kifupi, kinyang'anyiro cha Kibra, kinageuzwa kuwa patashika la siasa ya mchujo wa rais 2022 baina ya kinara wa ODM, Raila Odinga na kinara wa Tanga Tanga, Naibu rais William Ruto. Kwa sasa. Kulingana na kambi ya Raila (ODM), hakuna ubishi dhidi ya kiti cha ubunge cha Kibra, ni siasa ya kufa na kupona!

Mcdonald Mariga amekuwa mkuki moyoni mwa ODM kukiwa na wasi wasi wa mafungu ya wapigaji kura wa eneo bunge la Kibra ambalo linao mchanganyiko wa jamii tofauti. Hakuna upande ama chama ambacho kinao uhakika maalum kwamba mgombea wake anaweza kushinda akitegemea kura za jamii yake tu.

Hatua ya ODM kuwaleta pamoja wagombeaji walioshindwa kwenye mchujo ni kuhakikisha wamethibiti umoja wa jamii kwanza ya Waluo kabla ya kunyenyekea jamii nyingine wapiga kura wa Kibra. Ujumbe uwazi hapa kwamba mbunge mwendazake Ken Okoth alikuwa ni wao kijamii na kichama hivyo hakuna haja ya wagombea wengine kubaki nje ya kampeini za ODM kumsakia Imran Okoth kura.

> **"Kinyang'anyiro cha Kibra, kinageuzwa kuwa patashika la siasa ya mchujo wa rais 2022 baina ya kinara wa ODM, Raila Odinga na kinara wa Tanga Tanga, Naibu rais William Ruto."**

### NASA yasuasua

Huku ODM, mmoja wa mzazi wa mrengo wa upinzani wa NASA ikingangana kutetea kiti chake cha Kibra, vinara wenza wa Raila, Moses Mudavadi, Moses Wetangula na Kalonzo Musyoka wamekazana kuhakikisha pia wamepata fungu la kura za Kibra kwa vyovyote vile baada ya kila mmoja kuwasilisha mgombeaji wake.

Jambo hili pia limeshawahi kumdhuru Raila Odinga kwa kukosa kiti cha Embakasi na Kalonzo Musyoka akashinda kupitia mgombeaji wake wa Wiper. Safari hii hataki aibu kwa chama chenye ufuasi mkubwa kama ODM kikose kutetea kiti chake kwa kushindwa mashinani.

Kusuasua kwa muungano wa NASA hatahivyo, kunampa nguvu naibu wa rais William Ruto ambaye amemwelekeza Mcdonald Mariga kama fimbo ya kutaka kumchapia Raila na hundi yake ya "Handisheki" akimtumia vile vile kasuku wa Kakamega, Bonny Khalwale kama kiongozi wa kampeini za Mariga.

Mwanya upo baina ya wagombeaji wa Raila na Mudavadi ambapo kura huenda zikagawanywa kijamii ikiwa Eliud Owalo (ANC) na Imran Okoth (ODM), wataanza kuzigawa kura kijamii. Owalo hali kadhalika huwezi kumweka katika uzani wa chini kwani ameshawahi kuwa mkaribu wa Raila na mbinu huenda akawa amezihami kulipiza kisasa cha kisiasa.


Kivumbi cha mwisho

Kufikia mwisho mwa Septemba bila shaka watatu, Imran Okoth, Mcdonald Mariga na Eliud Owalo ndio wanaoonesha ishara kamili kuwa kivumbi kitakuwa baina yao. Hii ni ishara hatari kwa Musalia Mudavadi na Raila Odinga kwa sababu ikiwa wagombeaji wao ndio watakaokuwa maarufu kwenye kampeini hizi, hali hiyo inaweza kuwaponza.

Watabiri wa masuala ya siasa wanasema kuwa endapo kampeini zitanoga zaidi kwa hawa watatu (Okoth, Owalo na Mariga), basi itakuwa ni aidha Owalo ama Mariga kulingana na mchezo wa siasa ulivyo mijini kama kaunti ya Nairobi.

**Mbunge wa Malindi akashifiwa vikali katika makundi ya kijamii ya Wachonyi, baada ya kutoa matamshi ya matusi dhidi ya mbunge wa Kilifi Kusini, Ken Chonga kwenye mkutano wa Naibu Rais William Ruto eneo la Mtwapa."**

# JUMWA ASUTWA KUMWITA CHONGA KIKARAGOSI





JUU: **Ken Chonga** CHINI: **Naibu Rais William Ruto akiongea na mbunge wa Malindi Aisha Jumwa wakati wa hafla ya kuchangisha fedha eneo la Mtwapa.**

https://t.me/magazeti

**NA ALFRED KITI**

Mbunge wa Malindi Aisha Jumwa amekashifiwa vikali katika mitandao ya kijamii na makundi ya jamii ya wachonyi ambao ndio wengi katika eneo bunge la Kilifi Kusini baada ya kutoa matamshi ya matusi dhidi ya mbunge wa Kilifi Kusini Ken Chonga.

Jamii ya wachonyi wakiwemo viongozi, wazee, akina mama na vijana wamemshutumu vikali Aisha Jumwa kwa madai ya kuwatumia baadhi ya wanasiasa kutoka jamii ya Wachonyi kuwagawanya kisiasa na pia kueneza chuki kati yao.

Hii ilitokana na matamshi ya Ken Nyale kwenye hotuba yake wakati wa mkutano wa kuchangisha pesa ulioongozwa na Naibu Rais William Ruto mjini Mtwapa mwishoni mwa wiki kusisitizia kauli ya Mustafa Idd kwamba waakazi wa eneo bunge la Kilifi Kusini hawakuchagua kiongozi mwaka 2017 bali walichagua kikaragosi, yaani sanamu.

Wachonyi walikashifu sana wakisema hawatakubali kugawanywa na Aisha Jumwa maana kauli ya Ken Nyale kuthibitisha kuwa Ken Chonga mbunge wa sasa ni kikaragosi ikinuia kuleta chuki na mgawanyiko katika jamii ya Wachonyi.

Aisha ambaye alikiasi chama cha ODM kilichompa uongozi wa eneobunge la Malindi na kujiunga na kundi la Tangatanga la Naibu Rais Dr. William Ruto amejitokeza kimasomaso na kuwakashifu viongozi wenzake wa mrengo wa ODM huku akiwatusi na kuwaita "Ndutsi" neno kwa lugha yake ya Kigiriama linalomaanisha mtu mjinga asiyejifahamu.

Jumwa alikariri tamko la Mustafa Idd kwamba mbunge wa Kilifi Kusini ni Kikaragosi yaani sanamu jambo ambalo halikufurahiwa na wafuasi wa Ken na jamii ya Wachonyi kwa ujumla.

Licha ya Naibu Rais kumkabidhi Aisha mwanasiasa Ken Nyale washirikiane naye katika kampeni za kumpigia debe Kilifi, Mama Jumwa ameonekana kumpigia debe mbunge wa zamani wa Kilifi Kusini Mustafa Idd.

Wakati wa Hafla hiyo ya kuchangia pesa makundi ya kina mama na vijana iliyoongozwa na Naibu Rais Dr. William Ruto huko Mtwapa ambako ndilo shina la kura za Kilifi Kusini, Aisha Jumwa alimtusi mbunge wa eneo hilo Ken Chonga na kumtaja kuwa kibaraka wa Gavana wa Mombasa, Ali Hassan Joho ambaye kazi yake ni kupapasa ndevu za gavana huyo anayejiita Sultan.

Sio tu Ken Chonga aliyetusiwa na Aisha bali pia Seneta wa Kilifi Stewart Madzayo alitajwa kuwa mtu bure ambaye hakufaa kuchaguliwa.

Matamshi ya Jumwa yamewakera sana wakaazi wa eneobunge la Kilifi na hasa jamii ya Wachonyi ambao wamewataka viongozi waliotusiwa kujitokeza na kumjibu Jumwa.

Aisha Jumwa hata hivyo amekanusha madai ya kwamba anampigia Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Pwani Mustafa Idd na vilevile kusema kauli aliyoitoa Mtwapa dhidhi ya Mbunge wa Kilifi Kusini Ken Chonga ni hatua ya kujibu matusi waliyoyatoa viongozi wa ODM wakati wa kampei za uwakilishi wa wadi ya Ganda huko Malindi hivi majuzi.

Awali siku ya Ijumaa, Naibu Rais William Ruto alizindua mradi wa usambazaji umeme sehemu za mashambani unaofahamika kama Last Mile katika kijiji cha Kitsoeni, eneobunge la Kilifi Kusini tarafa ya Chonyi akiandamana na mbunge wa Malindi Aisha Jumwa.

La kushangaza ni kwamba hakukuwa na kiongozi yeyote wa kisiasa kutoka Kilifi Kusini hususan tarafa ya Chonyi aliyehudhuria hafla ya Kitsoeni huku ikibainika kwamba Jumwa aliyekuwa akiongoza msafara wa Naibu Rais aliwambia viongozi wenzake kwamba Ruto hangefika Kitsoeni na hivyo viongozi wote wakamsubbiri Ruto Mtwapa alikoenda kuongoza harambee ya kuchangia pesa makundi ya kina mama na vijana.

Ilitarajiwa kwamba viongozi wa kisiasa wakiwemo wale walio na nia ya kuwania viti vya kisiasa kama vile aliyekuwa mshauri wa kisiasa wa Naibu Rais William Ruto, Anania Mwaboza, Mfanyibiashara Michael Tinga, mwandani wa Ruto Ken Nyale na waakilishi wa wadi kutoka eneobunge la Kilifi Kusini wangehudhuria hafla iliyoongozwa na Ruto hapo Kitsoni, la kushangaza ni kwamba hakuna kiongozi wa eneo hilo hata mmoja aliyehudhuria.

Hatua ya Jumwa ya kuwatusi viongozi wa Kilifi Kusini hasa Jamii ya Wachonyi akiwemo Seneta Stewart Madzayo ilionekana wazi kuwa njama yake fiche ya kuonyesha kwamba Jamii ya Wachonyi haimthamini wala kumtambua Naibu wa Rasi William Ruto hatua ambayo wadadisi maswala ya kisiasa wanasema ni jambo la kawaida kwa mwanasiasa kumpaka matope mpinzani wako.

Ken Chonga ni miongoni mwa wanasiasa ambao wametangaza nia yao ya kuwania wadhifa wa Ugavana Kilifi.

Mbunge huyo wa Malindi ambaye tayari ametangaza azma yake ya kuwania kiti cha Ugavana wa Kilifi mwaka 2022 ameanza kuweka mikakati ya kampeni za uchaguzi ujao ikiwa ni pamoja na kuwawaleta karibu wanasiasa anaopania kushirikiana nao kwenye kampeni hizo wakiwemo naibu wake na wabunge watakaomuunga mkono.

Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Pwani, Mustafa Idd ambaye Aisha alimpigia debe zaidi wakati wa mkutano wa Ruto huko Mtwapa anaonekana kuwa kipenzi cha Jumwa awe Naibu wake mwaka 2022.

Kinyang'anyiro cha Ugavana Kilifi kinaelekea kuwa baina ya makundi mata-

> **"La kushangaza ni kwamba hakukuwa na kiongozi yeyote wa kisiasa kutoka Kilifi Kusini hususan tarafa ya Chonyi aliyehudhuria hafla ya Kitsoeni."**

tu, Kundi la Tangatanga likiongozwa na Naibu Rais Dr. William Ruto ambaye tayari amemchagua Aisha Jumwa, Kundi la ODM la Raila Odinga ambapo mfuasi wake sugu Ken Chonga ametangaza nia nya kuwania na Kundi la Kieleweke la Rais Uhuru Kenyatta linalolenga macho yake kwa aliyekuwa mbunge wa Malindi Gideon Mung'aro.

Wadadisi wa maswala ya kisiasa wanasema kwamba siasa za matusi ambazo zimelaaniwa vikali katika mitandao ya kijamii ni jambo la kawaida mafahali wawili wa kisiasa wanapomenyana.

Ziara ya Ruto eneo la Pwani ilianzia Tana River akafanya mikutano ya harambee Kilifi na kukagua miradi ya maendeleo ya serikali ya Jubilee, akaelekea Kwale na hatimaye kumalizia Taita Taveta.

Kote alikoenda alihubiri maendeleo ikiwa mbinu yake ya kuwashawishi wapiga kura kumuunga mkono katika harakati zake za kuwania wadhifa wa Urais mwaka 2022.

Ruto aliwarai wapiga kura hasa Kilifi Kusini ambako chama chake cha Jubilee kilipata kura chache mno kuacha msimamo wa kuabudu chama kama dini na waone maendeleo yanayoletwa na viongozi.

Huu ni mwanzo tu wa taswira ya mambo yanavyotarajiwa wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2022 huku ikiwa ni nusu tu ya muhula wa miaka mitano wa uongozi wa kisiasa ulioanza mwaka 2017.

# Hapo napo!

Gavana wa kaunti ya Taita Taveta Granton Samboja atoa amri ya kusimamisha utoaji wa leseni za biashara kwa maduka yanayouza muguka, aina ya Miraa inayojulikana sana.

Alisema uamuzi huo wake umepelekewa na malalmiko kutoka kwa wakaazi ambao wanasema utumiaji wa miraa umesababisha ukosefu wa kazi kwa vijana wengi.

"Wamama wamekuwa wakilalamikia kwamba hatujali ustawi ya vijana wao. Nimesikia kilio chao na nikaamua kuzuilia utoaji wa leseni hizo,"alisema Samboja.

Alikuwa akiwahutubia wakaazi wa Werugha kaunti ndogo ya Wundanyi siku ya Jumamosi.

Samboja alisema wiki mbili zijazo ataweka timu yake itakayozunguka na kuhakikisha kwamba hakuna yeyote anayeendelea na biashara hio.

Vilevile, alisema wakaazi wamezua hofu juu ya maswala ya afya kati ya vijana wanaotumia ulevi huo.

Mary Mwakio, mkaazi wa Wundanyi aliiomba serikali kuweka kituo cha marekebisho kwenye kaunti hio kwa kuwa asilimia kubwa ya vijana wamenaswa na madawa ya kulevya.

"Licha ya miraa, kaunti hii imejaa madawa ya kulevya ambao watoto wetu wanaotumia. Tunaomba serikali iweke kituo cha marekebisho kama kweli wa nataka kuangamiza janga hili la utumiaji wa madawa ya kulevya,"alisema.


Hata hivyo, Kinyua King'ori, mwenyekiti wa jamii ya wameru wanaoishi Taita Taveta alipinga uamuzi huo wa Gavana kupiga marufu ya biashara ya miraa.

King'ori alisema uamuzi huo hauko katika sheria za kaunti na hivyo basi hautatekelezwa kamwe.

"Huki akinadi kuwa vijana huenda wakawa wameathirika na utumiaji wa muguka, ni makosa sana kwa Samboja kutoa muelekeo pasi kutengeneza sheria itakayo guide hilo," King'ori aliiambia Pambazuko.

Alimtaka Gavana huyo kushughulikia pombe zote haramu zinazowauwa mamia ya vijana kabla ya kuanza vita visivyoeleweka dhidi ya wanabiashara.

King'ori alisema jamii hiyo inayoendesha biashara ya miraa kwenye kaunti hio itatoa jibu lao punde tu watakapopewa notisi ya kuacha kuuza kichocheo hicho.




# *Tuheshimu taasisi za ndoa kuthibiti wake bila taharuki ya wake wenza*

https://t.me/magazeti

Leo nazungumzia kuhusu suala la taasisi ya ndoa. Nimeguswa sana na matukio ya hivi punde na visa kadha wa kadha kuhusiana na mauaji, matukio na kawama baina ya nyumba ama ndoa za watu wa tabaka tofauti.

Mara twasikia mume ama mkewe kabadilishiwa mume mwingine ama mke mwingine. Pia twasikia mara bwana amemuua mke ama mke kamuua bwana kutokana na sababu moja au nyingine. Swali ni je, ulimwengu umepasukia wapi kiasi cha kutuweka kwenye fikra hizi mbovu?

Taasisi ya ndoa ni muhimu sana n ahata wakati mababu wa mababu zetu walipokuwa na wake ama mabibi zaidi ya mmoja, kweli walikuwa na sababu zao kufanya hivyo. Tuheshimu taasisi za ndoa ili tuweze kuthibiti wake zaidi ya mmoja bila ya taharuki kutoka kwa wake wenza kama ilivyokuwa nyakati za zamani.

Taasisi ya Ndoa imeheshimika sana hapa Barani Africa tangu jadi kabla ya chimbuko la Madhehebu ya Kikristo na Kiisilamu karne ya 17Bc.

Mifumo ya Jamii nyingi hapa Africa inawaruhusu waume kuwaoa wake wapatao 4 na Zaidi mradi tu mume ana uwezo wa kukidhi mahitaji ya familia yake. Kwa mda mrefu watangulizi mababu zetu wameweza kudhibiti ndoa za wake wengi bila taharuki kutoka kwa wake wenza.

Kumekuwepo pia njia maalum ya kusuluhisha migogoro katika ndoa inayoongozwa na familia maalum iliyotwikwa jukumu la kuwalea wanandoa wachanga kwa kuwapa ushauri nasaha na kutatua ugomvi baina yao.

Kadri miaka inavyosonga changamoto katika Taasisi hii ya Ndao zimekithiri na kuwafanya wanandoa kuchukua maamuzi ya kuogofya ambayo yamewatia matatani huku kwao ikiwa ni njia ya kipekee ya kusuluhisha malumbano tu.

Kutoka hatua ya mahusiano ya kirafiki hadi matayarisho ya kuchumbiana kumetokea tofauti baina ya wadau na hatimaye mauti husalia kwenye kumbukumbu ya jamaa na marafiki.

Ni mapema mwaka huu ambapo mwanafunzi wa kike katika Chuo Kikuu cha Moi huko Eldoret Ivy Wangechi alishambuliwa na mpenziwe kwa shoka na kuuawa kinyama mchana kisa kikiwa eti kukosa kujibu mawasiliano yake kwenye simu ya rununu licha ya kumpa usaidizi wa kifedha siku zote akiwa chuoni.



HASSAN M'MBETSA

Kilichoshangaza ni kuwa Ivy alishambuliwa kwa shoka na kisu na Mpenziwe Kinuthia anayeaminika kusafiri kutoka mji wa Thika hadi Eldoret kutekeleza unyama huo mwezi Aprili mwaka huu. Kinuthia ametiwa nguvuni na anasburi kuamuliwa kwa kesi ya mauaji dhidi yake.

Visa kama hivi vimeendelea kushuhudiwa nchini na kwa wakati mmoja mfanya biashara Joe Irungu maarufu kama Jowi alifikishwa kizimbani kwa tuhuma za kumuua Bi Monica Kimani mnamo mwezi wa Septemba mwaka uliopita kwenye makaazi yake yaliyoko mtaa wa Lamuria Kilimani Jijini Nairobi kwa ushirikiano na mpenziwe Jacky Maribe, kesi dhidi yao inaendelea kusikilizwa kayika mahaka kuu jijini Nairobi.

Aidha mauaji baina ya wanandoa yameendelea kushuhudiwa kutoka maeneo mbali mbali nchini katika eneo la Lukiyani county ya kakamega Maghraibi mwa nchi, Mme amemuua mkewe kwa kushuku kuwa na mahusiano nje ya ndoa na jirani wao.

Bwana Noah Inyangala mwenye umri wa miaka 34 alimshambulia mkewe Bi. Metrine Nasimiyu kwa kile kilichotajwa na majirani kuwa ugomvi wa kinyumbani baina yao licha ya kuwepo kwa ndoa yenye amani kwa muda wa zaidi ya miaka minane.

Vile vile kisa kama hicho kimeshuhudiwa mwezi Juni mwaka huu Mjini Kitui. Mwili wa kiongozi wa vijana katika eneo hilo Bwana Benjamin Kinyali ulipatikana ukiwa umechomeka vibaya sana baada ya kuwepo ugomvi baina yake na mkewe.

Taarifa za uchunguzi wa polisi zilibaini kwamba mkewe Bwana Kinyali alikuwa kwenye mahusiano na mtu aliyeaminika kuwa jambazi sugu. Kama hatua ya kulipiza kiasi, Kinyali aliamua kumchumbia mke wa jamaa huyo na kukawa na mashindano ya kutuma picha kama njia ya kumkwaza mwenziwe anapomuona mpinzani wake anavyojivinjari na mkewe.

Aghalabu kisa kilichowatia mwili baridi wanandoa ni kile cha hivi punde ambapo mwili wa bwanyenye mmoja mzaliwa wa Uholanzi Tob Cohen ulipatikana umefungwa na kutupwa ndani ya mtaro wa majitaka nyumbani kwake Kitusuru Jijini Nairobi, kisa ambacho kumewaacha wengi Vinywa wazi ikizingatiwa kwamba bwenyenye huyo aliripotiwa kupotea kwa muda wa siku 40 kabla mwili wake kupatikana ukiwa umeanza kuoza.

Baadhi ya Marafiki wa Bwana Tob Cohen waliozungumza na wanahabari wakati wa shughuli za kuondoa mwili wake wanahoji kuwa bwanyenye huyo alikuwa amewaarifu kwamba maisha yake yamo hatarini kutokana na ugomvi baina yake na mkewe Bi. Saraha wairimu Kamotho ambaye anashikiliwa katika korokoro ya Gere a la Langata na anatarajiwa kufikishwa mahakamani kujibu mshtaka ya mauaji dhidi yake baadaye mwezi huu.

Je ni nini chimbuko la matatizo haya ya ndoa? wanasaikolojia wanahoji kuwa hali mbaya ya kiuchumi, mzongo wa mawazo na tamaa ya kutithi mali ni baadhi ya mambo yanayochangia sana visa vya mauaji ndani ya ndoa kuongezeka kila kuchao.

Pambazuko

Gazeti la Pambazuko linasimamiwa na: Hassan M'mbetsa Beja - Mhariri mtekelezi | Mohammed Thabit - Mhariri msaidizi | Is'haq Gunga Chea - Mkarabati wa lugha |
WACHANGIAJI MAKALA - Alfred Kiti | Lolani Kalu | Tom Kazungu | Brivian Simiyu | Francis Mwaro | Mghoi Mzae | Rachel Kavumbi | Juma Mrisho

KENYA NATIONAL SPELLING BEE 2019

Proudly brought to you by: Festive

# THE SPELLING BEE SHOW, Now on KTN Home

Catch all the buzz, as Kenya's best spellers battle it out for the title of Spelling Champion 2019




**Every Saturday from 10-11am**

VEDA Start imagining

Ting Ting Bubble Gum

KENTAINERS innovative solutions • for water & sanitation

Crown

dt dobie

I&M Bank

Capital Markets Authority

https://t.me/magazeti

KCB BANK

ktn

# I've built my business the way I've built myself. Can my strength match the Lions'?

**Watch me pitch next week Tuesday at 8PM.**

Regulated by the Central Bank of Kenya KCBgroup #KCBLionsDen KCBgroup KCBgroup

LIONS' DEN

# Wabunge wazitaka kaunti kuwajibika kabla ya kuomba pesa



Mwenyekiti wa baraza la magavana nchini Wycliffe Oparanya wakati alipoongoza wenzake katika mchakato wa kushinikiza mfuko wa kaunti kutoka kwa kamati za Bunge na Seneti.

**NA EDWIN NYARANGI**

Wabunge Watano kutoka eneo la Gusii wamelitaka Baraza la Magavana kuonyesha jinsi fedha walizopokea kwa miaka saba iliyopita zilivyotumika kabla ya kuitisha nyongeza kutoka asilimia 15 hadi 45.

Wakizungumza na Pambazuko mjini Kisii wabunge hao walisema kuwa mpango wa Magavana nchini kuunga mkono kura ya maamuzi kupitia mchakato wa Ugatuzi hautafanikiwa kwa vile wengi wao wametumia fedha za umma kwa njia mbaya.

Mwenyekiti wa Kongamano la Wabunge wa Gusii Joash Nyamoko alisema kuwa mchakato huo unaopigiwa debe na Gavana wa Meru Kiraitu Murungi na Gavana wa Makueni Kivutha Kibwana utapingwa na wakenya wengi.

Nyamoko alisema kuwa Magavana wengi wanahudumu kwa kipindi chao cha pili na wangependa kuonekana wanapigania kuongezwa kwa fedha kwenye majimbo yao ilhali wengi wamefuja fedha zilizonuiwa kutekeleza miradi ya kuwanufahisha wananchi.

### Utajiri wa haraka

"Magavana wengi walikuwa wanaishi maisha ya kawaida miaka minane iliyopita, la ajabu ni kuwa wengi wao wanamiliki mali yenye dhamani ya Mabilioni ya pesa huku watu wao wakihishi kwenye lindi la umaskini," akasema Nyamoko.

Mbunge wa Bomachoge Borabu Zadock Ogutu alisema kuwa yeye hawezi kuunga nia hiyo ya magavana mkono hadi pale serikali za majimbo zitakopotumia fedha wanazopokea kutoka kwa hazina kuu na ushuru unaokusanywa kwa njia nzuri.

"Mbali na barabara chache ambazo zimefanyiwa ukarabati, serikali za majimbo mengi nchini hazidhihirishi jinsi zimekuwa zikitumia mabilioni ya pesa ambazo wamepokea kwa miaka saba iliyopita," akasema Ogutu.

Mbunge wa Nyaribari Chache Richard Tongi alisema kuwa ingawa anaunga mkono serikali za majimbo kupata fedha zaidi kutoka kwa serikali kuu ilikuwa jambo la muhimu kwa serikali hizo kuhakikisha zinaanzisha miradi ya maendeleo itakayowafaidi wakenya.

Tongi aliziomba serikali za majimbo kote nchini kushughulikia maswala ya ufisadi katika maeneo yao kabla ya kuwashawishi wakenya kuwa wanahitaji fedha zaidi kwa vile kwa sasa Wakenya hawajatosheka kuwa wanahitaji fedha zaidi.

"Maafisa wengi wa ngazi za juu katika majimbo mengi nchini wanaishi maisha ya anasa ilhali wananchi wanakosa mahitaji ya msingi maishani, wanapaswa kutuonyesha ni vipi wamekuwa matajiri wa kupindukia kwa muda mfupi," akasema Tongi.

Mbunge wa Dagoreti Kaskazini Simba Arati alisema kuwa litakuwa jambo ngumu kwa majimbo kupata fedha zaidi kwa vile Magavana wengi wametumia pesa walizopokea kwa njia ya ubadhirifu na itakuwa makosa makubwa kuwaongeza fedha zaidi.

> "Magavana wengi waliishi maisha ya kawaida miaka minane iliyopita. Wengi wao sasa wanamiliki mali yenye dhamani ya mabilioni ya pesa."

Arati alisema kuwa iwapo kila wadi nchini ingepata Sh 100 Milioni kwa ajili ya maendeleo kila mwaka kutoka kwa serikali za majimbo na ziweze kutumika kwa njia nzuri wakenya wangeweza kufikia upeo mkubwa wa kimaendeleo tangu ugatuzi uzinduliwe miaka saba iliyopita.

"Mchakato wa kura ya maamuzi ya Ugatuzi unaoungwa mkono na magavana hauendi popote kwa vile Magavana wengi wanahudumu kipindi chao cha pili ilhali hakuna lolote la maana wamefanya kwenye majimbo yao," akasema Arati.

Mbunge wa Bomachoge Borabu Alpha Miruka alisema kuwa yeye haungi mkono mchakato huo wa magavana kwa vile katika maeneo mengi nchini miradi mingi inayo onekana ni iliyofadhiliwa na hazina ya maeneo bunge nchini.

Miruka alisema kuwa majimbo mengi yanatumia nyingi ya fedha wanazopewa kwa mishahara na marupurupu ya wafanyikazi badala ya kutekeleza miradi ya maendeleo maeneo mbalimbali huku wakenya wengi wakikosa kuona umuhimu wa ugatuzi.

"Magavana wanaounga mkono mchakato wa kura ya maamuzi ya ugatuzi wanafaa kujitokeza watuambie jinsi walivyotumia mabilioni ya pesa walizopokea kutoka kwa hazina kuu tangu kuzinduliwa kwa ugatuzi," akasema Miruka.

### Kwa muhtasari

Gavana wa Meru Kiraitu Murungi na Gavana wa Makueni Kivutha Kibwana wanapigia debe mchakato wa kura ya maamuzi ya Ugatuzi ili kuongeza fedha kwenye majimbo. Baraza la Magavana nchini na Umoja wa Mabunge ya Majimbo nchini yameanzisha mchakato wa kura ya maamuzi ya ugatuzi ili kuongeza fedha zinazopeanwa kwenye majimbo kutoka asilimia 15 hadi 45.

Mchakato wa kura ya maamuzi ya ugatuzi ni watatu baada ya ile ya punguza mizigo inayopigiwa debe naye Dkt Ekuru Aukot na ile ya kundi la kuunda Madaraja nchini inayoungwa mkono naye Rais Uhuru Kenyatta na Waziri Mkuu Raila Odinga.

https://t.me/magazeti

# Serikali yalaumiwa kwa mimba na ndoa za mapema

**NA BRIVIAN SIMIYU**

Serikali imelaumiwa pakubwa kwa visa vya mimba na ndoa za mapema katika eneo la pwani kutokana na hatua ya serikali kuondoa sheria ya adhabu ya kiboko shuleni.

Kulingana na mzee wa Kaya Diani Abdallah Boga amesema kuwa licha ya serikali kuondoa sheria hiyo kwa kigezo cha kulinda haki za mtoto, hatua hiyo imechangia pakubwa ongezeko la mimba na ndoa.

"Serikali imefanya makosa kwa kuondoa sheria ya kumwadhibu mtoto na ndio maana visa vya watoto kupachikwa mimba vinazidi kuongezeka," alisema Boga.

Kwa upande wake mzee wa Kaya kutoka kaunti ya Lamu Ali Ndokolani amesema kwamba wazee katika kaunti hiyo wameanzisha mpango wa kuwapima watoto mimba.

Ndokolani amedai kuwa mpango huo unalenga kukabiliana na visa vya mimba za mapema miongoni mwa watoto wa shule.

"Tuliamua tuje na mpango wa kuwapima mimba watoto wa kuanzia darasa la tatu hadi darasa la nane ili kuhakikisha kwamba wako salama," alisema Ndokolani.



Naibu gavana wa Kwale Fatuma Achani.

Wakati huo huo, Ndokolani amelaani vikali kitendo cha wazee kuhusishwa pakubwa na tuhuma za uchawi.

Amedokeza kwamba hatua hiyo inatokana na tamaa ya watoto kutaka kurithi mali za wazazi wao.

Hata hivyo, naibu gavana wa kaunti ya Kwale Fatuma Achani ameitaka jamii katika eneo la pwani kuwa mstari wa mbele kulinda haki za mtoto wa kike.

Achani ametaja umuhimu wa jamii kumlinda mtoto wa kike huku akiwataka wazee kuwathamini akina mama ili kuiwezesha jamii kupiga hatua.

"Wazee wana jukumu kubwa la kuwalinda watoto wa kike na kuwathamini akina mama ili waweze kuheshimiwa katika jamii," alisema Achani.

Wakati huo huo, mzee wa kaya kutoka kaunti ya Kilifi Karisa Wa Fagio amewalaumu vikali wazazi kwa kutelekeza majukumu yao ya kuwalinda watoto wa kike.

Ametaja ukosefu wa malezi mema kuwa sababu inayochangia visa vya mimba za mapema katika jamii.

"Mtoto anapokosa mwelekeo ni makosa ya mzazi kushindwa kumlea vizuri. Kwa nini tumewacha majukumu ya kuwakanya watoto wetu?" aliuliza Karisa.

Haya yanajiri kufuatia ongezeko la visa vya mimba na ndoa katika eneo la pwani.

Viongozi hao walikuwa wakizungumza wakati wa kuadhimisha sikukuu ya Chenda chenda iliyofanyika katika eneo bunge la Msambweni kaunti ya Kwale.

Sikukuu hiyo huadhimishwa kila mwaka ili kusheherekea tamaduni na mila za wamijikenda.

# Kesi za dhulma ya watoto zaongezeka

**NA BRIVIAN SIMIYU**

Imebainika kwamba kesi za watoto kudhulumiwa kimapenzi katika eneo la Diani kaunti ya Kwale haziripotiwi kutokana na hatua ya wazazi kuamua kutatua kesi hizo kinyumbani.

Kulingana na afisa wa shirika la kijamii la kutetea maswala ya watoto katika kaunti hiyo Zipporah Nyawera, wazazi wa kiume wamelaumiwa pakubwa kwa kukosa kuripoti kesi hizo.

Nyawera amedai kuwa hali hiyo inaathiri pakubwa mchakato wa kutafuta haki licha ya akina mama kuwa mstari wa mbele kuwatetea watoto wao.

"Kuna kesi nyingi za watoto za dhulma ya kingono japo kesi hizo hazichipuki kwani mara nyingi akina baba hukataa kupaza sauti zao licha ya akina mama kutaka haki ya watoto wao," alisema Nyawera.

Afisa huyo pia ameipongeza idara ya mahakama ikishirikiana na idara ya watoto kaunti ya Kwale kwa kuanzisha mpango wa kuzisikiliza na kuziamua haraka kesi hizo za watoto.

Amesema kuwa tayari jumla ya kesi 42 zinazohusiana na dhulma ya kimapenzi dhidi ya watoto zimeamuliwa katika kipindi cha wiki moja tangu kuzinduliwa kwa mpango huo.

"Nashukuru majaji wetu wa Kwale kwa kuchukua hatua ya kuziangazia na kuzishughulikia kwa haraka kesi zote za watoto," alisema Nyawera.

Hii inajiri baada ya kubainika kwamba kesi nyingi za watoto huchukua muda mrefu kuamuliwa mahakamani.

Wakati huo huo, mkurugenzi wa idara ya watoto kaunti ya Kwale Steven Gitau amewataka wazazi kutokubaliana na uamuzi wa kutatua kesi za watoto kinyumbani. Gitau aidha amewashauri wazazi kuzingatia sheria ili kuhakikisha kwamba watoto wanaopitia dhulma ya kimapenzi wanapata haki.

Septemba 18 - 24 | Pambazuko

# Chemichemi za wiki



https://t.me/magazeti

"Kijana mmoja awalilia Wazee wamurai babake ili amregeshee bibi yake ambaye alinyang'anywa na mzazi wake aliyeamua kumchota mkaza mwanawe."

Uk 10

# ADAI HAKI BAADA YA BABAKE MZAZI KUMNYANG'ANYA MKEWE



# ADAI HAKI BAADA YA KUNYANG'ANYWA MKE NA BABAKE

https://t.me/magazeti

**"Mzazi amua kumchota mkaza mwanawe eneo la Malava, Kakamega na sasa kijana awalilia wazee wamurai babake ili amregeshee bibi yake aliyenyang'anywa."**

**NA DENNIS AVOKOYWA NA ALPHA BURUDI**

Mwanaume mmoja kutoka kijiji cha Mukongolo eneo bunge la Malava kaunti ya Kakamega anadai haki kutoka kwa wazee wa eneo hilo baada ya babake mzazi kumnyanganya mke na kisha kufumaniwa akishiriki na yeye tendo la ndoa hata baada ya wawili hao kuzaa watoto pamoja.

Kulingana na mdokezi wetu mshukiwa ambaye ni babake mwathiriwa amekuwa na mazoea ya kuwanunulia wawili hao mvinyo kila jioni hii ikiaminika kuwa moja kati ya njama alizokua nazo za kumkwachua msichana huyo mara hii akimpumbaza na kumnunulia pombe kupita kiasi na kisha kutoweka na mkewe kabla yake kufumaniwa akichovya kisima cha wenyewe.

Akizungumza baada ya tukio hilo, mwathiriwa kwa jina Peter Barasa (mtoto wa mzee huyo) anadai kuwa amekuwa akishuku mienendo za babake, mara hii akimleweshwa kupita kiasi na aliporejea na fahamu zake alimkosa mkewe na babake waliokuwa wameandamana naye, na moja kwa moja akafuliza hadi kwake huku akipitia karibu na boma la babake alikoskia minongono ya wawili hao akidhani kuwa wanapiga gumzo na mkewe atarejea chumbani ila aliamshwa usiku wa manane na makelele kutoka kwa boma la babake na alipokimbia kushuhudia alivunjwa moyo na kisa alichosimuliwa.

"Amezoea kutununulia pombe, sikujuwa alikuwa anajipendekeza kwa mkewangu, niliporejewa na fahamu sikuwaona lakini niliskia wakiongea kwa nyumba ya babangu nikamshwa usiku wa manane na makelele kwa boma la babangu kuenda kutazama nikata mke wangu akipigwa na dadangu baada ya kufumaniwa wakila uroda kwa kitanda cha babangu," Akasema Barasa

Akithibitisha kisa hicho mzee wa uko huo wa abahenyu joseph muruya amesema kuwa wawili hao walifumaniwa na mtoto wa mzee huyo (dadake mwathiriwa) aliyekuwa ameenda kuchukua simu yake iliyokuwa kwenye nyumba hiyo nyakati za usiku na kuwapata wawili hao wakishiriki tendo hilo kwenye kitanda cha mzee huyo wakati mama mwenye nyumba alikuwa amesafiri.

"Wawili hao walipatwa wakishiriki mapenzi na dadake mwathiriwa alipokuwa akienda kuchukuwa simu kwa iliyokuwa kwa moto kwa nyumba ya babake," Akiongeza kuwa aliyefumaniwa alilazimika kuchukua watoto na kutorokea nyumbani kwao.

Aidha Barasa alidai baada ya tukio hilo mkewe pamoja na watoto wake walimwacha na kuhamia kwa babake huku akibaki na upweke.

"Alichukuwa vitu vyote vya nyumba na kuhamia kwa babangu," Akasema Barasa.

Hata hivyo, Barasa ameamua kutalakiana na mkewe huku akitaka uko kumhamisha baba yake kulingana na mila na desturi ya jamii hiyo.

## Wabadilishana wake

Kama ilivyonakiliwa kwenye vitabu takatifu kwenye dini ya kiislamu na kikristu, anayepata mke amepata kitu kizuri na mke mwema hutoka kwake Mwenyezi Mungu jinsi mwimbaji wa nyimbo za injlili Bonny Mwaitege alivyosema.

Ni kipindi kipi hicho utampata mwanamume kuamua kubadilishana mke na mwananamume mwenzake? Basi ukistaajabu ya Musa ya Firauni utayaona Busia eneo la Magharibi humu nchini

Tukio hili lilijiri wakati mke alimuacha mume wake aliyekuwa kajaliwa naye wana wawili na kuenda kujiunga na mume wa mke mwingine.

Millicent Auma ambaye amekuwa akiishi na mumewe Christopher Bwire katika kitongoji cha Siroba kijijini Matayos alikata kauli na kuondoka kwenye ndoa yake na kujiunga na Kevin Barasa.



**Zawadi ya ndoa baada ya Kevin Barasa kukabidhiwa mke huyu Millicent Auma kutoka kwa mumewe Christopher Bwire katika kitongoji cha Siroba, Matayos kaunti ya Busia**

Bwana Barasa na bi Lillian Weta wameishi pamoja Kama mume na mke kwa miaka kumi katika kitongoji kidogo cha Namwitsula kijijini Butula na kujaliwa na wana watatu, hata hivyo, bi Weta ametoa madai ya kuwa ndoa yao katu haijakuwa na furaha ila vurugu na magombano yamekuwa desturi.

Anasema kuwa bwanake alirejea nyumbani usiku na Auma huku Auma akiwa amevalia koti la Barasa. Kabla ya bi Weta kusema lolote, Auma alimuamuru Weta aondoke kwenye chumba hicho. Amri nyinginge ikatoka Kwa barasa mumewe akimuamuru aende zake Kwa mumewe Auma akaoleke kule.

"Walikuja nyumbani mida ya saa Saba usiku na mume wangu, wakati huo sikuwa nimelala maanake mtoto wangu alikuwa mgonjwa.

Auma bila uoga akaniarifu yeye ni mkewe mume wangu kuanzia wakati ule" bi Weta alisema "mume wangu wakati uo huo akaniamuru niondoke niende nikamtafute mumewe Auma nioleke kwake, nilipomuuliza ikiwa jambo hilo halingemkwaza alisema mwanzo angefurahia kuona jambo hilo likifanikishwa.

Nilipowapigia ndugu na dada na kuwauliza hatima yangu, walisema nifanye nilivyokuwa nimeamrishwa." Weta aliongezea.

Ilipofika asubuhi anasema alienda kwa bwana Bwire na baada ya kufikiria doa lililokuwa kwenye ndoa yao akiwa na Barasa akamweleza alivyokuwa ameambiwa na Bwire akamwambia akarudi kwake arejee na vitu vyake pamoja na watoto waanze maisha.

## Yungali anampenda

Kabla ya taarifa hii ya Auma kuolewa na Barasa kupasua mbarika, Bwire alikuwa amemtafuta mkewe kwa udi na uvumba bila mafanikio.

"Siku hizi napata kila nachotaka na kulala usingizi wa pono tofauti na ilivyokuwa hapo awali, hata hivyo, katika siku zijazo, nina uhakika mmoja baina yetu, mimi au Barasa atajutia tendo hili maanake majuto ni mjukuu na huja kinyume." Barasa alisema.

Mzee Osuru kutoka maeneo hayo alisema ni jambo geni swala hili kutokea tangu enzi za mababu na ni mwiko mkubwa uliovunjwa unaohitaji tambiko la aina yake ili mambo yao na maisha yawe mema ila hamna jinsi wangefanya kuzuia wanandoa hao maanake hawakusikia la mwadini wala mteka maji msikitini.

# Matapeli wamekuwa kibao mpaka kwa mtandao




NA PASCAL MWANDAMBO

Ningelikuwa nimeondoka kwenda zangu nyumbani ila kwa ugomvi baina ya mhudumu wa baa na jamaa mmoja anayejulikana kama Chomelea. Jamaa huyu hufanya kazi ya kuchomelea vyombo vya plastiki vilivyopasuka; zikiwemo beseni, karai na zinginezo.

Mvutano ulisababishwa na tukio kwamba Chomelea alizidisha pombe na kisha kushikwa na usingizi. Katika hali hiyo, bwawa la Arror lilivunja kingo zake na punde alipoamshwa na mhudumu, kulikuwa na kijito chini ya meza.

"Hukuajiri mtu hapa wa kukusafishia mkojo, mlofa wewe. Hebu chukua dasta pale kwa kona usafishe uchafu wako ama nikunyanyue," mhudumu akamfokea Chomelea.

Nililipa bili yangu na kuanza



kuelekea steji nichukue teksi niende nyumbani. Ilikuwa saa nne usiku.

Punde tu nilipofika steji, jamaa mmoja tumezoea kumwita Sheikh alinikaribia na kuniamkua.

Muda kidogo baadaye, nilibaini kwamba alikuwa na habari kem kem ambazo alikuwa anataka zichapishwe magazetini.

Alinivuta kando kidogo na kunionyesha mkoba uliojaa mawe.

"Piga haya mawe picha uandike habari", Sheikh akaniomba.

Ingawa nilikuwa nimepata mvinyo kiasi cha haja, sikuwa mjinga asilani.Yaani kuandika habari ambazo hazina kichwa wala mkia.

"Naona tu mawe sioni kitu kingine cha ajabu hapa" nilimjibu Sheikh ambaye ni mmoja wa wakatia wasafiri tiketi kwenye ofisi ya kampuni moja ya mabasi.

Tuliketi kwenye benchi kisha akanaanza kunihadithia kilichotokea.

Alinielezea jinsi jamaa mmoja alivyoabiri matatu mjini Mombasa akiwa na majonzi tele akidai alikuwa amefiliwa na mtu wa ukoo wake mjini Taveta na hakuwa na nauli.

Jamaa huyo alidai kwamba angechukua hela kwa rafiki yake mjini Voi kulipia nauli kisha kuendelea na safari yake kuhudhuria matanga Taveta.

Mwenye matatu kwa ule utu wa Msamaria mwema, alikubali kumsaidia jamaa huyu.

Walipofika Voi, alimwomba dreva kumpa muda kidogo achukue hela kwa rafiki yake hapo karibu ndio aendelee na safari.

"Naomba muniangalie begi langu, narudi muda usio mrefu" jamaa huyo akamsihi mwenye matatu.

Kumbe hivyo ndio jamaa kuhepa na kupotea.Walingoja.. ng'oo.

Yamkini kituo cha mwisho cha tapeli huyu kilikuwa Voi ila hakuwa na nauli, ndipo akajitungia hadithi hii ya alfu- lela- ulela.

Mwenye matatu kufungua begi. Lahaula. Mawe yaliyofungwa kwa vifurushi!

Kisa hiki kilinikumbusha kingine nilihadithiwa na jamaa mmoja mwanafunzi wa chuo kimoja hapa nchini.

Kijana huyu alipatana na mrembo wa shani kwenye mtandao wa Facebook na baada ya muda wakaanza kuchati.

Baada ya muda usio mrefu, mrembo huyu alionyesha nia ya kuwa rafiki wa karibu na kijana huyu.

Jamaa alijiona kapata. Kulingana na wasifu wake kwenye Facebook, mrembo huyu alikuwa mhudumu kwenye hoteli moja maarufu mjini Mombasa.

Jamaa aliamua kufunga safari hadi Mwambao kukutana na kidosho huyu ambaye alikuwa wa kuvutia si haba, kulingana na picha iliyoandamana na wasifu wake kwa Facebook.

Hatimaye, jamaa aliwasili kwenye mkahawa alikokubaliana kukutana na windo lake mrembo, tabasamu likiwa limetanda usoni huku akichokora chokora smartphone yake.

Punde tu kulitokea jimama la umri wa makamo mrefu mweusi, mwenye pua yenye alama kama aliyechomwa na asidi.

Jamaa alifungua profile ya huyo mrembo na kumwuliza mama huyu, " Naomba unisaidie kama unamjua mrembo huyu.Tuliagana tukutane hapa".

Mama huyu alitoa tabasamu, akionyesha mapengo mawili na kimjibu, "Huyo ndio mimi.Hiyo ndio picha mimi hutumia kwa facebook. Karibu Mombasa"

Jamaa alipigwa na butwaa akakosa la kusema. Aliomba radhi kwenda haja ndogo na hivyo ndio kuhepa:Kijana alifikiri kapata kumbe kapatikana.

Ndio hali ilivyo.Kila mahali bidhaa gushi; dhahabu gushi, viongozi gushi, marafiki gushi.Matapeli na wanyonyaji.

Ndio maana sasa nimezoea kupokea zawadi hewa kwa simu yangu ya rununu baada ya kushinda raffle sijawahi kucheza hata kwenye ndoto.

Yote tisa kumi ni kwamba nipitapo mjini Voi sina hata muda wa kuchukua T-shirt zinazopeanwa bure, bora uwe na laini ya simu ya kampuni fulani.Baada ya kupokea T-shirt unaombwa utoe shilingi elfu mbili upewe simu ya rununu.

Kama huna unaambiwa eti toa shilingi mia tano ndio uchukue hiyo vazi.Bure imeshageuka kuwa gharama.Tuweni macho watu wangu.Si vyote vinavyong'aa ni dhahabu. Zingine ni sakafu za makamasi.

https://t.me/magazeti

# Umuhimu wa kitunguu saumu na asilia yake kwa afya

NA STEPHEN DIK

Kitunguu saumu au kitunguu thumu ni jamii ya vitunguu na hutumika zaidi kama kiungo kwa mboga na pia katika tiba, hasa inapotafunwa au kukatwa katwa na kuchemshwa.

Kitunguu saumu kiko katika familia ya Alliaceae na yaaminika kilitokea Asia ya kati na kuenea ulimwengu mzima.

Viambata vinavyopatikana kwa kitunguu saumu ni Vitamini C ambayo iko katika kiwango cha juu zaidi, Vitamini B6 na Manganese.

Kitunguu saumu hutibu magonjwa mbali mbali yasiyopungua 30 ikiwemo kusaidia yeyote aliye na matatizo ya nguvu za kiume.

Wanasayansi wamebaini kwamba kitunguu saumu hushughulika pakubwa

kuzuia mafuta kujikusanya na kuganda kwenye mishipa ya damu, ikiwemo ateri zinazopeleka damu katika uume wa mwanaume.

Damu inafaa kuteremka kwa urahisi hadi kwa mzinga wakati wa ngono, kumwezesha mwanaume kuwa mahiri kufika kileleni na kudumu kwa mda mrefu.

Wakati wa tendo la ndoa waeza tafuna kitunguu saumu lakini usitafune mda mfupi kabla ya ngono kwani ladha yake na harufu huwa sio nzuri kinywani.

Hivyo basi, kama wewe ni mwanaume, inashauriwa kuongeza kitunguu saumu mara kwa mara katika lishe yako na hatimaye utaona manufaa yake, itaimarisha afya ya mwili wako na matukio chumbani.



Kitunguu saumu hutibu baada ya kutumia kwa kati ya wiki mbili na mwezi mmoja pekee.

Katika kuandaa kitunguu saumu ya tiba, waeza katakata kama nilivyosema awali kisha wachemsha kwa dakika kumi na kunywa ikishapoa. Au pia waeza tafuna kwa kiwango kidogo sababu yaweza kudhuru ukila nyingi.

Ukianza kuumwa na kichwa baada ya kula kitunguu saumu kwa mda, unaweza kupumzika kwa siku mbili au tatu kisha uendelee tena.

Ugonjwa mwengine pia ambao unaweza kuzuiwa kwa kutumia kitunguu saumu ni ugonjwa wa Saratani ambayo sasa imekuwa tishio nchini Kenya.

Magonjwa kadha wa kadha ambayo yanaweza kutibiwa kwa kutumia kitunguu saumu ni kama vile Amoeba, minyoo na mabakteria wengine.

Kitunguu saumu tena hutibu Typhoid, mafua na malaria.

- Hutibu msokoto wa tumbo.
- Huondoa mabaka mabaka kwenye ngozi, huzuia kuhara damu (Dysentry).
- Husafisha njia ya mkojo.
- Hutibu kifua kikuu (TB)
- Hutibu kipindupindu.
- Hutibu upele.
- Huvunja vunja mawe katika figo.
- Hutibu mba kichwani.
- Huupa nguvu ubongo.
- Huzuia meno kung'oka, hutuliza maumivu.
- Hutibu maumivu ya kichwa.
- Hutibu kizunguzungu.
- Hutibu maumivu ya jongo.
- Huongeza nguvu mfumo wa mmeng'enyo wa chakula.
- Huongeza hamu ya kula,
- Huondoa gesi tumboni na pia kulisafisha tumbo, Hutibu shinikizo la juu la damu.
- Husaidia uthibiti wa kiwango cha sukari mwilini na kupunguza madhara ya kisukari.
- Pia kitunguu saumu kina umuhimu wa kuondoa sumu mwilini na kumpa mwanadamu nguvu za kuishi kwa miaka mingi.

Kitunguu saumu inasemekana kina madhara yake ikiwemo "allergy", kichefuchefu, kutapika na kuharisha lakini mtu anapoharisha kwa siku mbili au tatu mfululizo nafaa kufurahi na kushangilia sababu ni njia moja ya mwili kujisafisha.

Unapotumia kitunguu saumu kwa tiba, harufu mbaya ikiwa mdomoni yaweza kupunguzwa kwa kunywa maziwa, kunywa maji mengi au kutafuna karafuu. Inasemekana watu wa zamani walikula kitunguu saumu kwa wingi ndiposa wakawa wanaishi kwa miaka mingi duniani.

Kitunguu saumu kina manufaakwa mwanadamu aliye hai pekee na kwa wafu haina umuhimu wowote. Hekaya za kidini zinasema Wamisri walijua umuhimu wa kitunguu saumu kwa afya ya mwanadamu akiwa hai, kingi wao Farao (Firauni ) alipofariki walimwaga tani nyingi za kitunguu saumu kwa kaburi lake ili iweze kumsaidia kwa njia moja au nyengine lakini hakuna. Hii ni thibitisho kwamba kitunguu saumu kina manufaa kwa aliye hai pekee, tusibaki nyuma.

BUSTANI YA **MASHAIRI**

# Miaka mia tisa na tisini na tisa

**Mungu nakuinamia, mwanao ninakujia,**
**Mwilini kujazilia, nguvu kunizidishia,**
**Miaka yangu na pia, sana kunijazilia,**
**Miaka mia tisia, na tisini na tisia.**

**Miaka mia tisia, na tisini na tisia,**
**Mola naomba fikia, tena nakusujudia,**
**Maisha yaje ingia, miaka mia tisia,**
**Miaka mia tisia, na tisini na tisia.**

**Mengi nayatarajia, katika hii dunia,**
**Mimi sijatamania, kwa mapema kujifia,**
**Mipango ya kidunia, bado sijatimizia,**
**Miaka mia tisia, na tisini na tisia.**

**Macho sijafungulia, sijaona ya dunia,**
**Machache nimepitia, mengi nayatarajia,**
**Maovu ya kidunia, Mola kuniepushia,**
**Miaka mia tisia, na tisini na tisia.**

**Mimi Dik nakimbia, maisha nakimbilia,**
**Mbio ninazikimbia, ndani ya hii dunia,**
**Miaka kunifidia, umri kunibarikia,**
**Miaka mia tisia, na tisini na tisia.**

**Maneno najiimbia, leo ninafurahia,**
**Moyoni nashangilia, maisha najivunia,**
**Miaka iwe tisia, mia tisa na tisia,**
**Miaka mia tisia, na tisini na tisia.**

**Miaka iwe tisia, mia tisa na tisia,**
**Mola ninakusifia, dua naimalizia,**
**Maombi kuyasikia, shairi kunijibia,**
**Miaka mia tisia, na tisini na tisia.**

**MWALIMU MPENDA USHAIRI**

# Ngoma bado yaendelea

**Ngoma inaendelea,**
**Muchai apiga tumba,**
**Na memba waselelea,**
**Maungo ya yumba yumba,**

**Wengine wapalilia,**
**Ngoma izid kupamba,**
**Na baadh wavivia,**
**Memba sasa wapagawa!**

**Memba vumbi watibua,**
**Majad yame wabamba ,**
**Kuna mtu wa kuvia,**
**Na yule alo zagamba,**

**Yani mja kizulua,**
**Aso jua kujipamba,**
**Tucheze ngoma vizur,**
**Huku twatazama jua**

**Kuna hasira kujamba,**
**Na chuki zenye umbea,**
**Mambo haya ya kulumba,**
**Hayataki kuzembea,**

**‘Sidhan kuitwa mwamba,**
**Ni kupayuka kimbea,**
**Memba ngoma yarindima,**
**Tucheze tukitazama**

**Tucheze tukipekua,**
**Kutunga sio kuimba,**
**Kuna maneno murua,**
**Ukisema yatatamba,**

**Kuna nyimbo za umbea,**
**Ambazo hazina namba,**
**Wakatabahu taarab,**
**Memba tucheze vizuri.**

**MWALIMU MPENDA USHAIRI**

# Mambo haya zungulu pitu

**Sawa na ndumakuwili,**
**Mara huku mara kule!**
**Hajulikan mwayule?**
**Au mwahuyu rijali,**

**Si mtu ni duduvule!**
**Haja iva mwanamwali,**
**Mambo haya zungulu pitu**
**Memba tuelewe vipi?**

**Zikisongana kauli,**
**Huwatatiza wa kale,**
**Mwana kuwa ni fidhuli,**
**Ni aibu kwa wavyele,**

**Tabia za baradhuli,**
**Zitawatia upele,**
**Heri kutulia tuli,**
**Kuliko memba kubweka!**

**Kullko memba kufyoka,**
**Mambo bila kujadili,**
**Kuna maneno mwafaka,**
**Na tabia za kinduli,**

**Ni lini tutapevuka,**
**Tuwe kama maliwali?**
**Memba wanamangamanga,**
**Mawazo yavurugika.**

**Mawazo yakorogeka,**
**Ubwabwa sasa ugali,**
**Ajabu mbona twashuka,**
**Hatupand marijali,**

**Ni nini kimekoseka,**
**Busara au adili,?**
**Wakatabahu namaka,**
**Memba wana aibisha!.**



**TANGAZO: TUMA MASHAIRI YAKO KWA AIDHA BARUA PEPE : hmbetsa@gmail.com ama thabiti1964@gmail.com ama kupitia SMS/SIMU +254723068181.**

https://t.me/magazeti

BUSTANI YA **HADITHI**

# Machozi yawabubujika kwa kuiona maiti ya Farida



Na Ally Mwanyumba

INAENDELEA....

Ali Dzihunde, kachero kiongozi wa mda katika vijana wale wane wanochunguza wapi, kwa nini na nani alimpoteza Farida, alikuwa akimbebeleza kijana mchungaji mifugo asiende, asubiri kidogo.

Kijana mwenyewe alipogundua kuwa jamaa wale wanne ni kama wanauhusiano na polisi, alikuwa akitetemeka mwili mzima na jasho jembamba likidhihiri katika maungo yako, hasa bapa la uso. Alikuwa na wasiwasi wa kupita kiasi labda akihofia atapelekwa jela na kudhaniwa yeye ndo amemuuwa mwanamke yule.

"Baba atateta kwa nini nimepeleka mifugo kuchelewa nyumbani "kijana yule alisema kwa uoga.

"Usijali ... wewe huna ubaya ... usiogope .... tutakupeleka tukamweleze baba ako... subiri tu kidogo... tubebe hii maiti halafu utaenda... kuna zawadi nzuri tutakupatia." Ali Dzihunde akamrahi.

Kijana alimtazama kachero yule bila ya kuyaamini maneno yake.

Kwa mbaali katika barabara hiyo ya mchanga upande wa mjini iliyoelekea huku makao ya mayatima, kulionekana vumbi ikitibuka. Ilidhihirika ni gari kama mbili zikifuatana mbio sana.

Bado vijana wanne wapelezi walikuwa imara na chonjo pale maeneo iliyokuwepo maiti ya msichana yule mrembo. Waligundua kuwa ni gari za usalama, utumishi kwa wote, polisi.

"Wamefika "Rashid Bendago aliwajulisha wenzake kama ambao hawakuziona gari hizo. Gari ya mbele ilikuwa kama Nissan matatu , ndani ikiwa na watu kama sita pamoja na dereva . Ya nyuma ake ilikuwa aina ya Land Rover iliyobeba kikosi cha "gonga mlizaa" au ua kabisa, yaani kikosi cha "hit squad".'

Walikuwa kama askari kumi walioshika bunduki kubwa aina ya Ak-47 wakiwa tayari kulenga yoyote waliyemdhani kuwa adui au jambazi.

Kabla hazijasimama vizuri gari hizo, askari waliokuwa ndani ya Land Rover waliruka chini ghafla kama tumbiri huku wakielekeza midomo ya bunduki za Ak-47 pande zote. Ilibidi makachero wote wanne waonyeshe ishara maalum za kijeshi ili wajitambulishe kuwa wao pia ni usalama kwa wote.

Kijana mchungaji alianza kulia. Hakuamini bahati yake alipoona kikosi kile cha usalama. Ni mara yake ya kwanza kuwaona ana kwa ana maafisa wa usalama. Eee, kumbe wanatishia wakiwa kazini? Kijana yule alihisi kama haja ndogo na kubwa pale pale, na kuanza kujivuta akitaka kuponyoka mbio, lakini Alii Dzihunde alikazanisha mashiko ya mkono wake.

"Usi"ogope jomba ... mimi niko, hakuna shida." Alizidi kumrahi Alii Dzihunde, kachero kiongozi wa mda wa upekuzi ule.

Makamo, wa chini yake komanda mkuu katika idara kuu ya upelelezi, afande Jackson Madume alishuka mara moja kutoka kwa Nissan iliyoongoza msafara huu. Alikuwa chonjo, imara, tayari kwa lolote huku akijipapasa kiunoni taratibu kama bunduki yake iko maali pake.

Alitupa macho huku na kule kuyaangaza maeneo haya ambayo yamedhihiri kuwa hatari kwa usalama. Alimwona Rashid Bendogo akiegemea gari yao Rav4 kando ya barabara akiwasubiri tayari. Kwa mbali, kama maili tatu hivi, majengo ya makao ya mayatima aliyoyaona kumanda yule mdogo Jackson Madume.

"Wapi... ni wapi afisaa?" Alimuuliza Rashid Bendogo upesi upesi.

"Pande hii... bosi." Rashid Bendago alijibu kwa kuchangamka na kuelekea njia ya miguu kuliko na wenzake pamoja na maiti ile ya mwanamke.

Rashid Bendago, kijana kachero mpole aliongoza njia. Komanda mdogo Jackson Madume nyuma yake akifuatia na Mzee Babad na mhariri Feisal ambao wote hawa waliitwa baada ya komanda mkuu Daud Madonga kupokea simu ya kwamba kuna mwanamke amepatikana karibu na makao yale ya mayatima.

Kuna maafisa wawili pia walioshuka kwenye Nissan ile waliobeba mabegi madogo, nao walifuata msururu wa msafara huo uliokuwa ukielekea mahali maiti ilipo.

"Ni huyu hapa bosi," Rashid Bendago aliotesha kidole mahali maiti ya mwanamke ilipokuwa imelala kifudifudi.

Wote waliizingira maiti ya mwanamke yule wakiwa wanahisi kama mzizimo katika viwiwili vyao?

"Mzee...?... Ndie huyu? Unaweza kumtambua mwanao? Komanda mdogo Jackson Madonga alimuuliza Mzee Babad.

"Ni yeyee.... Aaaah..jamani.. mke wangu Faridaaa kwani umekosa nini.. aaah!

Ahmed Darwesh aliekuwa karibu aliangua kilio cha nguvu kabla Mzee Babad kujibu swali la Komanda Jackson Madonga.

Mzee Babad, babaake marehem Farida, alijikaza kidogo kisha akaanza kwikwi za kilio taratibu huku akijishika kichwa kwa mikono yake. Mhariri Feisal Majid wa gazeti la pekupeku alihisi machozi yakibubujika kama maji ya mfereji baada ya kumtambua mwandihi wake Farida.

Baba, mume na mwaajiri wa Farida watokwa na

Huzuni ilienea maeneo yote pale, hata miti ilionekana kutotingishika wala tagaa na majani kupepea. Kila kiumbe aliekuwa karibu alihisi damu ikienda kwa kasi. Isipokuwa mumewe marehemu farida, Ahmed Darwesh na Mzee Babad na mhariri Feisal, waliokuwa wakilia kwa uchungu.

"Kwani umekosa nini kwa mungu mke wangu mpaka wakakufanya hivi?" Ahmed Darwesh mumewe marehemu Farida alisikika akibweka kwa kilio na huku akijisukasuka kama mtu alieshikwa ni mapepo!

"Chukueni hawa ndugu waliofiwa.... weka kwa gari muwapoze kilio... nani..? Wapi wale maafisa nimekuja nao..?.. chukua picha sehemu yote hii.. alama za vidole kwa ile begi ya marehemu tunataka pia.. weka vizuri begi yake itasaidia uchaguzi?" Komanda mdogo Jackson madume alitoa amri zote hizi mara moja.

Maafisa wa usalama waliokuwa na mabegi waliotoa kamera na vitambaa vya kushikia begi lile la marehemu, Halafu wakapiga picha mara moja.


"Ita wale maafisa kwa landrover waje na machela yaku bebe hii maiti waweke kwa gari." Alizidi kutoa amri Jackson Madume na kijasho chembamba akikihisi mwilini mwake.

Shughuli zote zilitendeka kwa kasi na kwa ujuzi kama walivyozoea kazi hizi maafisa wale. Wakati maiti ya Farida ilipokuwa ikibebwa, ilionekana kama ubavu wa kulia ulikuwa unaanza kuoza na kutoa harufu ya uvundo! Waliziba pua zao, na komanda madume alitazama kando kuhepa harufu ile.

"Kuna gari ndogo chini kule kwa maporomoko bosi ... inaonekana ni teksi ya kampuni ya Mombasa raha iliyombeba." Alii Dzihunde kachero msaidizi alimjulisha bosi wake.

"Aaaiii... hii ilikuwa vita kamili...? ... Ayiyiyiii...wacha tuitishe ndege ya helikopta kule makao makuu.." Alisikika Komanda Jackson Madume na kutoa simu yake ya mkononi.

INAENDELEA....




https://t.me/magazeti

# Madaktari wa kienyeji wataka wenzao gushi wafurushwe

**NADENNIS AVOKOYWA**

Imekuwa ni kawaida, kila ukitembea mijini au vijijini hutakosa kuona vibango vya matangazo ya madaktari wa kienyeji,wakitangaza kutibu magaonjwa ya kiajabu ajabu ikiwemo kurudisha mpenzi, kurudisha nguvu za kiume pamoja na kukinga boma dhidi ya maadui kati ya magonjwa mengine tangazo ambazo zimewasababishia wengi hasara wakijaribu kutafuta huduma kwa madaktari hao.

Ni kutokana na hili ndio muungano wa madaktari wa kienyeji kaunti ya Kakamega wameitaka kampuni ya kusambaza umeme ya KPLC kuwakomesha kubandika vibao hivyo kwenye miti yao.

Muungano huo ukiongozwa na kiongozi wao Arnold Ambutu wanadai matangazo hayo yamepelekea kuibuka kwa madaktari gushi wa kienyeji wanaowalaghai wakaazi na kuhatarisha afya ya wengi huku sifa zao zikiaribiwa.

"Kuna madaktari wameikuja hapa Kakamega kutoka sehemu mbali mbali kama vile Uganda, Narok na sehemu zingine wanajiita madaktari wakienyeji hatuwajui na ndiyo maana tunataka wapigwe marufuku," akasema Arnold.

Akitumia mfano wa jamii ya wamaasai, kiongozi huyo alidai kuwa jamii hiyo inajulikana kaunti ya Kakamega kama walinzi nyakati za usiku lakini inashangaza kuwaona mchana wakitembea na vibuyu vya madawa wakiwalaghai wakaazi kwamba madawa hayo yanatibu magonjwa yote.

Aidha alisema madawa hayo yanahatarisha afya ya watu wengi huku madaktari hao gushi wakiongezeka na kusababisha vifo.

"Madawa hayo yanadhuru afya na kuleta magonjwa mengine mengi ya tumbo kando na saratani na kutuharibia kazi," akasema Arnold.

Hata hivyo amewatahadharisha wazazi dhidi ya kutumia dawa hizi kwa binti zao kuavya mimba akizihusisha na sababu ya kuongezeka kwa vifo kwaa mabinti hao pamoja na kuwaambukizi magonjwa ambayo hayaeleweki.

Aliongeza kuwa haja yao ni kupata pesa na hutoweka kila wakikusanya na kunusia madhara madhara kwa watumiaji wa dawa zao.



Mbunge was Changamwe Omari Mwinyi akifungua shule ya msingi ya Magongo wiki iliyopita.

# KRA, KEBS matani kwa kuzuia ukaguzi wa mizigo bandarini

**FRANCIS MWARO**

Halmashauri ya ukusanyaji ushuru na Shirika la kutathimini ubora wa bidhaa nchini Kebs, yanashutumiwa kwa kutoyapatia masharika mengine nafasi ya kufanya kazi zao za kukagua mali ambazo huingizwa ndani ya bandari ya Mombasa.

Mashirika haya mawili yameleekezewa kidole cha lawama baada ya meli ambazo ziliingia hivi karibuni na mizigo ya nafaka, ambayo yadaiwa ilikuwa si salama kwa utumizi wa binadamu.

Shehena hiyo ambayo iliingia majuma matatu yaliyopita yadaiwa kuwa ni ya kiongozi mwenye haiba ya juu serikalini.

Shirika la ukaguzi wa kiafya la Port Health linadai kunyimwa nafasi ya kukagua mali za nafaka pamoja na za EPZ ambazo zilikuwa hazikifikisha kiwango cha kutumiwa na binadamu.

Akizungumza wakati was ufunguzi wa shule ya msingi ya Magongo mbunge wa Changamwe Omari Mwinyi ameyataka mashirika haya mawili kuyapa nafasi mashirika mengi ya kukagua mizingo kufanya kazi zao, ili kuhakikisha vyakula vinavyoingia ni salama kwa matumizi ya binadamu.

Ukarabati wa shule pamoja na ujenzi wa afisi ya walimu uligharimu shilingi milioni 13.2.

"Kuna mashirika mengine ndani ya bandari yetu yananyimwa nafasi ya kufanya kazi zao, kwa sababu ya kulinda mali ya 'wakubwa' ili ipitishwe bila kukaguliwa na mashirika ya kiafya, yanayoangalia iwapo mali hiyo ni salama kwa binadamu, kwa hivyo nasema hapa KRA na KEBS yanastafaa kuruhusu shirika la Port health na mengineyo kufanya kazi zao," akasema Mwinyi.

> **"Hatutakubali ukora huo kuendelezwa ndani ya bandari yetu kwa madhumuni ya kuwalinda watu wachache."**

Mbunge huyo amesema magonjwa mengi yanayowakumba binadamu mara nyingi yanasababishwa na vyakula ambavyo vimeharibika na ambavyo havijakaguliwa hivyo basi kuwadhuru binadamu.

"Kuna magonjwa mengi kama saratani, na iwapo vyakula vinapokaa siku nyingi katika usafiri wa baharini, mara nyingi huharibika na vyakula hivyo vinapaswa kukaguliwa ipasavyo, ili kulinda afya za wanadamu. Hatutakubali ukora huo kuendelezwa ndani ya bandari yetu kwa madhumuni ya kuwalinda watu wachache," akaongeza.

### Nafasi za kazi bandarini

Nafasi za kazi ambazo hutolewa katika bandari ya Mombasa yadaiwa haziwanufaishi wakazi wengi wa hapa pwani, kwani baadhi ya viongozi huziuza nafasi hizo kwa minajili ya kujinufaisha wao wenyewe.

Mbunge huyo wa eneo Changamwe anasema kunazo nafasi 100 za kazi ambazo kila mbunge wa eneo la Pwani alipewa kuwanufaisha wakazi wa maeneo bunge yao, lakini nafasi hizo zinauziwa watu wakutoka sehemu nyengine.

"Sisi viongozi nafasi za ajira tunazopewa, wengi wetu tumekuwa na tabia ya kuuza nafasi hizo, ilhali huku kwetu kuna vijana wengi wasiokuwa na ajara, mbona tuuze nafasi hizo ? Hawa vijana wetu wengi ambao wamesoma tutawapeleka wapi?" akauliza Mwinyi.

Nafasi nyingi za ajira zimepotea baada ya shirika la reli nchini kuamuru makasha kubebwa na reli ya kisasa kuenda Nairobi, hali ambao Mwinyi ameitaja kuwa ya kupunguza nafasi za kazi kwa wingi kwani vijana wengi wameachishwa kazi.

Ameilaumu serikali kwa kutunga sheria ambazo zitawakandamiza wakazi wengi kwa kuwakoseshwa ajira.

"Hatupingi serikali lakini ikiwa imeleta sheria za kuumiza wakenya hatutakubali. Leo hii vijana wengi waachishwa kazi na kampuni ambazo zinasafirisha mizigo kwa sababu mizigo yote inabebwa na reli ya kisasa, jambo ambalo hatutalikubali na tutaendelea kulipinga," akasema.

# Wakulima hawaelimishwi kuhusu madawa haribifu

**NA MOHAMED SEIF**

Matumizi ya madawa ya kikemikali ya kupambana na wadudu kwenye kilimo yameruhusiwa kuendelea kiholela bila kujali athari za kimsingi zinazo sababishwa na madawa hayo ambayo pia ni sumu kwa mazingira na afya ya binadamu.

Utepetevu huu wa udhibiti umeachwa kukithiri kutokana na ushawishi wa makampuni makubwa hususan ya kimataifa yanayo tengeneza madawa haya kwa hoja kwamba uzalishaji wa chakula cha kutosha na chenye ubora haiwezekani kufanikika pasipo matumizi ya madawa ya wadudu.

Mtazamo huu umeelezwa na mwanaharakati wa masuala ya ukulima endelevu ambaye pia ni balozi wa Route to Food Initiative (RTFI), shirika ambalo linajihusisha na vuguvugu la kupendekeza mfumo wa kilimo asili kama mbinu mbadala ikilinganishwa na matumizi ya madawa ya kemikali.

Emmanuel Atamba anasema ukulima wa kutegemea madawa ya wadudu ni mfumo ambao athari zake haribifu ni nyingi mno. Ukulima huo ndio umependekezwa kwa kisingizio kwamba kilimo asili hakiwezi kutegemewa kuzalisha mazao ya kutosheleza.

"Mafichuzi yalotokea hivi karibuni kuhusu chakula kinacholiwa humu nchini yanaonyesha mfumo wa uzalishaji chakula ambao haufai na ambao unahitaji hatua za haraka sana kurekebishwa na kubadilishwa," anasema Atamba.

"Wale wanaopigia debe mfumo huu wa uzalishaji chakula wanahoji kwamba utumiaji wa madawa ya wadudu sio tatizo iwapo wakulima watafuata maelekezo ya utumiaji wake kama yalivyo chapishwa. Hoja hii sio sahihi hususan ukizingatia muktadha wa jamii zetu."

Mwanaharakati huyo anaeleza kwamba maelekezo ya utumiaji wa madawa haya huandikwa kwa lugha ya kitaalamu ambayo wakulima wengi hawaielewi. Anasena kwamba ukaguzi ulowahi kufanywa mnamo 2013na kitengo cha masuala ya chakula na wanyama cha Muungano wa bara Ulaya ulibainisha kwamba wakulima huwa hawafuati maelezo ya madawa hayo.

Uchunguzi huo pia ulionyesha kuwa maelezo mengine ya matumizi ya dawa hizo yalikuwa na mapungufu katika maelekezo ya utumiaji.

"Hii inatuonyesha kwamba kampuni na wauzaji wa madawa haya hawatoi elimu ya kutosha kwa wakulima kuhusiana na matumizi yake salama," anasema Emmanuel Atamba.

Analalamika kwamba maafisa wa ukulima katika serikali za kaunti pamoja na Bodi ya Kudhibiti Madawa ya Wadudu hawafikii watu mashinani inavyo paswa kwa minajili ya kutoa mafunzo. Hivyo basi, upungufu wa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi ya madawa haya unazidisha hatari ya wakulima kuathirika.

Atamba alikuwa akiongea kufuatia ufichuzi wa hivi majuzi kwamba hadi asilimia 32 ya viungo vilivyomo kwenye madawa mbalimbali ya wadudu humu nchini ni madawa ambayo yamepigwa marufuku kutumika katika nchi za Ulaya.

Muungano wa bara Ulaya ilipiga marufuku hiyo kutokana na madawa hayo kuwa ni sumu kwa afya ya binadamu pamoja na mazingira.

Ufichuzi huo ulotolewa kwenye ripoti ya mashirika mbalimbali husika yakiwemo RTFI, Biodiversity and Biosafety Association of Kenya (BIBA-K), Organic Agriculture Network (KOAN) na Resources Oriented Developemnt Initiatives (RODI) pia ulionyesha kwamba kuna bidhaa 24 za madawa kama haya yanayo uzwa humu nchini huku bidhaa hizo zimethibitishwa kuwa na uwezo wa kusababisha saratani. Bidhaa nyengine nazo zilithibitishwa kuathiri uzazi wa binadamu.

Kitengo cha kitaifa kinacho husika na usalama wa bidhaa Kenya Plant Health Inspectorate Service, pia kiliripoti mnamo 2018 kwamba chembechembe za madawa ya wadudu yalipatikana kwenye aina kadhaa za mboga zilizochukuliwa kutoka maduka mbalimbali na masokoni.

https://t.me/magazeti

UKULIMA

# Madhara ya kutumia biringanya kwa wingi



Na Ishaq Gunga Chea

Kama tulivyosema katika maelezo yaliyotangulia kuhusu tunda la biringanya, kwamba ni tunda lenye manufaa mengi kwa mwanadamu kwa sababu ya kuwa na vipa nguvu vya kila aina na lishe thabiti kwa kuwa linabeba aina nyingi za vipa nguvu, ni wazi kwamba kila kilicho na manufaa hakikosi madhara au hasara.

Tunda hili lina madhara likiliwa kwa wingi, kwa hivyo watumiaji wa tunda hili wanapaswa kulitumia kwa busara. Makala haya yanasimulia baadhi ya madhara yanayotokana na kulila tunda hili kupita kiasi.

**Kwa akina mama**

Kwa sababu tunda hili lina chembe chembe zinazoongeza kima cha mkojo, akina mama waja wazito wanashauria kutolitumia mara kwa mara, kwa sababu linasisimua ada zao.

Mbali na hayo tunda hili lina chembe chembe ambazo husaidia katika matibabu ya hofu inayotokana na kuingiliwa na ada kwa wanawake hao. Ijapokuwa hilo ni la manufaa kwa mwanamke, lakini manufaa hayo huleta madhara kwa wanawake wenye uja uzito.

Tatizo jengine ni kwamba tunda hili kwa sababu ya kuwa na wingi wa vitamini, madini, lishe yenye nyuzi nyuzi kwa wingi, na vipa nguvu vinginevyo ambavyo ni vya manufaa kwa afya zetu, kwa mwanamke mja mzito husisimua chembe chembe ambazo zinapomsababishia kupata siku zake za kike, hatimaye humfanya akaavya uja uzito wake.

Kwa hivyo akina mama waja wazito wanashauriwa kuepuka kulitumia tunda hili mara kwa mara, na wanahimizwa kwenda kutafuta ushauri wa daktari kuhusu utumiaji wa tunda hili. Tunda hili kadhalika lina uwezo wa kusababisha asidi tumboni kwa hivyo wanawake waja wazito wanashauriwa kulitumia kwa uchache.

Tunda hili kadhalika linaweza kusisimua madhara ya allergy na kusababishia kuvimba kwa umio, kuchafukwa na moyo, kuhisi kuwashwa na kupata vipele. Hata hivyo madhara yoyote yanayotokana na kula tunda hili yana matibabu yake, lakini kama unapokula tunda hili unapata allergy basi inafaa uliepuke.

Taarifa iliyochapishwa katika gazeti moja la Uingereza linayoshughulikia masuala ya matibabu inasema, biringanya lina chembe chembe zinazojulikana katika lugha ya kitaalamu kama nicotine ambayo humfanya mtu akawa na uzoefu wa kupindukia wa kula vitu vyenye chembe chembe hizo, kama vile tumbaku.



Mlo wa biringanya

Lakini taarifa nyingine iliyochapishwa katika gazeti la New York Times inasema ingawa Biringanya lina chembe chembe hizo za nicotine, nicotine hiyo ina asidi ambayo kimuundo iko kama ile ya tumbaku, lakini haina madhara ya kumfanya mtu azowee kula biringanya kama inavyomfanya mtafunaji tumbaku ama mvuta sigara.

Kinyume cha ilivyo nicotine, chembechembe zinazofanana na nicotine katika biringanya hazileti madhara yoyote kwa miili yetu, na ni kiasili muhimu cha chembe chembe za niacin ambayo ni vitamini nzuri kwa ngozi ya mwili na utaratibu wa neva.

Hata hivyo wataalamu wanasema ili uwe salama kiafya, ni bora utumie tunda hili kwa kipimo ili upate manufaa yake muhimu kwa mwili wako.

Wataalamu wanasema wingi wa madini ya potassium na lishe nyuzi nyuzi ni hatari, na ingawa wataalamu wanasema madini na lishe hizo ni zenye manufaa kwa afya ya mwanadamu, zinapokuwa nyingi mwilini kupita kiasi, zinaweza kuleta madhara kwa afya. Madini ya potassium yanapopita viwango vinavyohitajika mwilini, yanaweza kukusababishia kuumwa na tumbo, kutapika na kuzusha ugonjwa wa hyperkalemia.

Wakati huo huo wingi wa lishe nyuzi nyuzi unaweza kukusababishia magonjwa ya kufunga choo, kuharisha, kupata matatizo ya mwili kutochukua lishe, na mengineyo. Kwa sababu hii, unashauriwa kula au kutumia tunda hili kwa kiwango cha busara.

**Wakati wa kumeza madawa**

Kuna baadhi ya madawa ambayo yanapotumiwa mtumiaji wa dawa hizo hafai kula tunda hili la biringanya.

Dawa hizo ni zile za kukabiliana na dhiki za kiakili, za moyoni na pia, endapo mtu anatumia madawa ya kukabiliana na shinikizo la damu anashauriwa asitumie tunda hili. Hii ni kwa sababu tunda hili lina chembe chembe zinazojulikana kama tyramine ambazo huibana mishipa ya damu na hivyo basi kupandisha shinikizo la damu.

Wakati unapokwenda kufanyiwa chunguzi za kimatibabu, wataalamu wanasema usitumie tunda hili kwa saa sabini na mbili kabla ya kufanyiwa chunguzi hizo kwani huathiri matokeo yake. Hasa chunguzi zinazofahamika kama Carcinoid Tumors Test.

# Zimbabwe ni nchi ya kale yenye changamoto, historia ya kuvutia



Na Thabit Muhammad

Sambamba na kifo cha Robert Mugabe mmoja wa viongozi wa kale na alotawala sana. Leo tunangazia nchi yake.

Zimbabwe ni nchi iliyo kusini mwa Afrika iliyo katika ya mito miwili mikubwa ya Zambezi na Limpopo.Ni nchi ambayo haina bahari.

Zimbabwe inapakana na Afrika Kusini upande wa kusini na Msumbiji upande wa mashariki.Botswana iko magharibi na hali Zambia iko kaskazini mashariki.

Bendera ya nchi ina miraba ya rangi nyeusi, nyekundu, manjano na kijani. Ina upinde mweupe pembe ya kuhoto na nyota ya pembe tano.

Kauli mbiyu rasmi ya nchi hii inajijenga katika miito mitatu ya Kazi, Uhuru na Umoja. Wimbo wa taifa hili umesheheni mambo hayo ikiomba Mungu ibariki ardhi yake.

Jiji kuu la Zimbabwe ni Harare kwenye makao makuu ya rais, bunge, afisi za wizara, benki kuu, afsi za balozi na mashirika mbali mbali ya kitaifa na kimataifa.

Mbali na Harare iliyo na idadi ya watu milioni moja na nusu kuna jiji la pili kubwa yaani Bulawayo ikiwa na watu 653,331.Chitunguze ina watu 356,800.

Zimbabwe imegawanywa katika mikoa 10 ya kiutawala.Mikoa hii ni Bulawayo, Harare, Manicaland, Mashonaland Central, Mashonaland Eastern na Mashonaland Western.

Mikoa mengine ni Masvingo, Matabeleland Northern, Matabeleland Southern na Midlands. Mikoa hiii inatawaliwa kupitia kwa mifumo ya kingereza ikiwa na wakuu wa mikoa ilivyo Kenya.

Zimbabwe ina idadi ya takriban watu milioni 16 ikiwa na lugha takriban 16 hususan kiingereza, kishona na kindebele. Lugha zengine ni kichewa, kichibarawe, kisotho, kikhoison, kitswana, na kitowana. Aghalabu hizi ni lugha za kikabila.

Kabila kubwa kabisa lenye nguvu ni la Shona lenye idadi ya asilimia 80% ya wazimbabwe. Hili ndilo kabila la kiongozi wa muda mrefu marehemu Robert Mugabwe na mrithi wake Emmerson Mnangagwa.

Kabila la Ndebele asili yao ni Afrika kusini walipofurushwa na shujaa wa kizulu Shaka na kuja Zimbabwe ambapo walidhibiti uongozi Zimbabwe.

Kulikuwa na falme zilotawala Zimbabwe tangu karne 10 kama ufalme wa Zimbabwe, Mwenemutapa na Rozwi.

Wandebele waliofika na kutawala sehemu kubwa ya Zimbabwe walikuwa na shujaa wao Mzilikazi ambaye alirithiwa na mwanawe Lobengula.

Aidha utawala wa kikoloni ulianzishwa mwaka 1880 na kampuni ya bwenyenye Cecil Rhodes aliyekuja kupora madini ya Zimbabwe na kuleta masetla 200 kutoka Afrika Kusini.



Rais wa Zimbabwe Emmerson Mnangagwa.



Rais was kwanza wa Zimbabwe Robert Mugabe.

Uingereza ilitawala Zimbabwe na kuazimia kutowa uhuru lakini walowezi masetla wakajitangazia uhuru na kuwanyima wafrika asili nch yao.

Hali hii ilipelekea mchafuko kwani wafrika walienda msituni kupigania ardhi yao dhidi ya walowezi walioongozwa na Ian Smith.

Utawala huu wa walowezi ulishindwa na Zimbabwe kuwa huru huku Robert Mugabe kuwa Waziri mkuu mwenye nguvu na Rais Canaan Banana asiye na madaraka.

Mugabe alidhibiti sera za ujamaa dhidi ya ubepari wa kimagharibi.Alichukuwa hatua ya kuwapokonya ardhi wazungu na kuwarudishia wazalendo.

Hatua hii ya kuwapokonya wazungu ardhi ilianzisha uhasama wa nchi za kimagharibi dhidi Mugabe kwani damu nzito kuliko maji.

Nchi za kimagharib ikiwemo Marekani ziliwekea vikwazo Zimbabwe na kuishutumu kwa ukiukaji wa haki za kibinadmu na kuzima demokrasia.

Mnamo tarehe 30 Julai 2017 jeshi la nchi lilimuweka Mugabe kifungo cha nyumbani katika mapinduzi baridi ya kimyakimya.

Emmerson Mnangagwa aliyekuwa makamu wake aliyemfukuza alirudi toka uhamishoni na kuwa kiongozi wa chama tawala cha ZANU-PF akiwa kinara na Rais wa nchi.

Katika kura za tarehe 30 Julai 2018 Mnangagwa alimshinda Nelson Chemsa na kuwa rais mpya alochaguliwa kikatiba. Akiwa matibabu kule Singapore Mugabe alifariki akiwa na umri wa miaa 92. Alizikwa jumapili iopita katika mazishi yalohudhuriwa na viongozi wa Afrika akiwemo Rais Uhruu Kenyatta.

https://t.me/magazeti

SANAA **TURATHI** NA UTAMADUNI

# Miti ndio turathi ya zamani zaidi duniani



Na Lolani Kalu

Turathi ya zamani zaidi inayopatikana kwa urahisi duniani kote ni mti. Kila mahali kuna miti ambayo wingi wake hufanya misitu na maisha ya mwanadamu yameathiriwa sana na mti.


Ninasema hiyo ni turathi ya zamani zaidi inayopatikana kwa urahisi nikilinganisha na rasilimali zengine tulizorithi kutoka kwa mababu zetu kama vile vito vya thamani na madini.

Unapotoka hapo nje kwako bila shaka unauona mti hata kama si wa kiasili bali ni wa kigeni. Hata kama umegeuzwa kuwa nguzo ya kusambaza stima. Miti ya kiasili ambayo hurithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine inajulikana kwa majina na watu wachache katika kila jamii ambao walizingatia umuhimu wake na kuifanyia utafiti.

Wale wa kiasili huitwa waganga wa kienyeji. Wengine hawayajui majina ya miti mingi ya kiasili na faida zake na badala yake wanayajuwa majina ya kitaalamu ya miti ya kigeni kama wanayofunzwa shule.

Tokea hapo zamani mti ndio uliotumiwa kwa uhifadhi wa mazingira na kizazi kimoja baada ya kizazi kingine. Tuanzie wakati wa Nabii Nuhu aliyeamriwa na Mungu awaonye watu wa umma wake kuhusu gharika itakaowamaliza usipokuwa wale walioamini.

Alijenga Safina kwa kutumia mti mkubwa aliouchonga kwa muundo



Nabii Nuhu aliunda mashua yake kwa miti.

wa hiyo Safina na kumalizia kwa miti mingine mingi. Na sisi sote tumetokana na kizazi kilichobakia baada ya hiyo gharika iliyowaangamiza wote waliokaidi kwa mujibu wa Masahafu.

Tulihifadhiwa na turathi hiyo ya kiasili ambayo mpaka leo hakuna turathi nyengine yoyote inayoifikia kwa manufaa yake.

Tukizungumzia mababu zetu kabla ya kuja kwa wageni katika Bara la Afrika,walitengeza dawa zao za kiasili kutoka kwa mti. Magome ya mti yangechemshwa na kuwa dawa ya kuponya magonjwa mbalimbali.

Mizizi ya mti pia ilitumiwa kwa ajili hiyo hiyo tangu jadi. Majani hali kadhalika yalitengezwa dawa na mafusho na za kuoga kuondoa nuksi na magonjwa mengine.

Mbali na dawa ambazo tuligundua baada ya kwenda shule kwamba hata hivyo vidonge tunavyopewa huko hospitali vimetengezwa kutokana na turathi hiyo hiyo ya zamani Zaidi.

Mbali na dawa hata zile zinazotumiwa na wachawi ambazo hutokana na miti mitupu, mti ni chakula pia. Mti huzaa matunda ya kila aina ambayo hutumiwa kwa chakula na pia dawa za kukabiliana na hata saratani na ukimwi.

Kuna mengi ambayo yanatokana na miti ambayo lau tuyataje yote basi twaweza kuandika kitabu cha kurasa nyingi sana hasa tukichambua aina tofauti za miti na kule inakopatikana katika maeneo ya pwani na bara na milimani na mapangoni na mwituni na baharini.

Hapa tunaileta fikra ya umuhimu wa mti katika muktadha huu wa Sanaa Mila na Utamaduni. Kuhusu Sanaa, mti umetumika katika utengezaji wa ala mbalimbali za muziki zikiwemo zumari, zeze na vinubu mbali na gitaa na hata vijiti vya kupigia ngoma za kiasili ambazo zenyewe hutengezwa kwa miti na kumaliziwa kwa ngozi ya mnyama upande wa juu.

Muwindaji aliyerithi taaluma hiyo kutoka kwa babu yake hutumia mishale na mikuki na zana zengine chungu nzima ambazo hazitengezeki bila mti. Wavuvi hutengeza madau yao kutokana na miti na wakulima hali kadhalika pembejeo zao ni za bidhaa za miti.

Hata ukiileta fikra yako katika maisha ya kisasa utagundua kwamba asilimia kubwa ya vitu unavyotumia nyumbani kuanzia hiyo nyumba yenyewe unayoishi hadi samani na vifaa vya matumizi nyumbani, vyote umevirithi kutoka kwa mti. Na je mizinga ya nyuki?

Na wazungu je? Hata wao hali kadhalika. Magari yale ya kwanza yalitengezwa kutokana na mbao na mpaka sasa wao hutegemea vifaa vingi ambavyo vinatokana na miti.

https://t.me/magazeti

MALIMWENGU

## Arukwa na akili baada ya kumuua chatu huko Siaya

**NA STEPHEN DIK**

Tukio la kutisha limetokea katika soko la Ugunja kaunti ya Siaya baada ya kijana kufunga mzoga wa chatu shingoni na kuanza kutembea naye.

Alikuwa akitembea na mzoga wa chatu huku akiubusu na kuuramba kichwani kana kwamba ni peremende, aliogopesha watu zaidi.

Kijana huyo barobaro inadaiwa aliua chatu huyo kisha akarukwa na akili. Alitembea na mzoga sokoni huku akiongea mambo ambayo hayaeleweki kabisa.

Juhudi za wakazi kumuonya aache kutembea na mzoga wa chatu sokoni hazikufua dafu, alitishia kuzua vita.

Chatu huyo alikuwa amefugwa na mchawi mmoja wa eneo hili na aliuawa usiku akiwa malishoni.

Kisanga hiki kilisambaratisha shughuli za biashara sokoni. Mfanyibiashara mmoja mjini humu anayefahamika kama Edna Mung'ala alisema hajawahi kushuhudia kisanga kama hicho maishani.

Alisema kuwa tukio hilo la kuogofya litamfanya ashindwe kupata usingizi kwa wiki nzima. Kulingana na mzee Patrick Odhiambo Odok, mtu hafai kuua nyoka au mnyama yeyote aliyefugwa kwa sababu za uchawi.

Mzee Odok anasema chatu kama huyo aliyeuawa huwa kwa kawaida hadhuru mtu, ukikutana naye njiani mpishe aende zake.

Anaongeza kusema kwamba iwapo mtu atamuua mnyama aliyefugwa na mchawi, anafaa kuenda kumtupa mtoni ili aende na maji na kupotelea mbali.

Anazidi kusema kwamba mnyama huyo alifaa kutupwa mbali kabisa ili mchawi mwenyewe asiweze kumwona.

Anahoji kuwa iwapo angetupwa chooni basi mchawi angefanya juu chini na kubomoa kisha kumtoa.

Mzee mwengine anayefahamika kama mzee Paul Ogwang' aliingilia kati na kudai kuwa kijana huyo alipatwa na masaibu hayo kwa kukosa kuelewa.

Anasema iwapo kijana huyo angejua athari za kuua chatu huyo basi angempeleka na kumtupa mtoni aende na maji, ni vile hakujua ni chatuwa kufugwa.

"Mchawi akiona mzoga wa mnyama wake wa kazi basi hukasirika, ni lazima alipize kisasi na panaweza tokea maafa au mtu kurukwa na akili," mzee Ogwang' anasema.

Kwa sasa kijana huyo ametoroka nyumbani na anasakwa na watu wa familia yao.



MAMA **NTILIE**

## Jinsi ya kupika pilipili tamu ya kukaanga



Na Zulekha Khamis



**MAHITAJI**
**NYANYA 3 KUBWA**
**CHUMVI KIASI**
**PILIPILI 3 KUBWA**
**KITUNGUU THOM PUNGE 5**
**MAJI YA LIMAU AU NDIMU**
**KIPANDE 1**

**JINSI YA KUPIKA**

Anza kwa kusaga pamoja nyanya, pilipili, kitunguu saumu, weka ndimu na chumvi. Saga mpaka vilainike vyote kwa pamoja. Weka sufuria yako kwenye moto na weka mafuta ya kupika nusu kikombe. Anza na kupika tomato nzito vijiko vitatu vya chakula, hakikisha tomato inakaangika kwenye moto wa kiasi ama mdogo mdogo sana.

Weka pilipili manga kiasi, "currypowder" bizari kijiko moja kidogo, bizari ya pilau kijiko kimoja kidogo na kama utapenda unaweza kueka bizari ya mchuzi lakini si lazima.

Pika kwenye mafuta ama ukaange kwa muda wa dakika mbili mpaka tatu. Baada ya hapo weka mchanganyiko wako pilipili uloisaga mwanzo, hakikisha moto uwe kiasi ama pilipili inaweza kuganda kabla ya kuiva.


Ipike pilipili kwenye moto wa kiasi kwa muda wa dakika tano mpaka saba ama mpaka uone tomato pamoja na pilipili zimebadilika rangi.


Ziiva utaona rangi yake ni tofauti na rangi ambayo ilikua apo mwanzo, basi ukiona ivyo ujue pilipili yako imeshaiva na unaweza kuchuja ama kuyatoa mafuta ambayo hutoyaitaji.

Unaweza kuyatoa yote aa unaweza kutoa kiasi. Unaweza kutumia ayo mafuta kupikia kitu chengine.

Toa kwenye sufuria pilipili yako na ueke kwenye bakuli ipoe alafu unaweza kuiifadhi kwenye chombo cha mfiniko. Inaweza kukaa kwa muda wa wiki moja bila kuharibika kama sehemu sio ya joto ,ama kama utaweka kwenye friji inaweza kukaa sana.

# Subira yavuta kheri katika maisha ya Mkristu yeyote





Na Kasisi Ernest Eshamwata

Mwanzo 15:1 Nakusalimu katika jina lake Bwana yetu Yesu Kristo.

Natumai u buheri wa afya ndugu mpendwa. Leo tutazungumzia umuhimu wa kuwa na subira katika maisha ewe ndugu mkristo.

Subira ni mojawapo wa sifa za muhimu ambazo zinatiliwa mkazo kwa kudhihirika katika maisha ya mashujaa wote wa imani katika biblia.

Ibrahim, baba wa imani ni mfano mzuri kwa wanaokusudia kujifunza kuhusu sifa hii.

Kabla ya kuendelea zaidi, hebu nikupe mfano wa hivi punde kupitia kwa michezo ambapo wapenzi wa kandanda mtashuhudia kuwa hali ya kuvumilia na subira imeleta ufanisi kwa wanamichezo wengi. Vile vile ni vyema kufafanua kuwa kwa wanaokosa sifa hii mara nyingi mambo huenda mrama. Wao huishia kupoteza tumaini.

Huingiwa na hamaki na hasira ya haraka. Hatimaye Baraka huwaponyoka! Ndiyo maana wahenga wakasema hasira hasara.Timu ambazo wachezaji wake wlikosa subira katika michuano ya bara Afrika ambayo iliandaliwa Misiri, hazikupata taji, kuna baadhi ya wachzanji walitangulia kufungwa goli lakini wakajizati na baadaye wakashinda.

Wasomi wa Biblia, mnafahamu bara bara kuhusu shujaa wa imani Ibrahimu.

Mmwanzoni akijulikana kama ABRAMU hakuwa amejaliwa kupata mrithi. Hilo linasumbua kweli kweli na kumrai Mwenyezi Mungu.

Sawa tu na mimi, nawe kuna mambo yanasumbua na kufanya tuwe na mafadhaiko mengi. Ukosefu wa ajira, kufeli mtihani mara ya kwanza, kukosa mchumba, kukosa wateja katika biashara n.k.

Katika kitabu cha mwanzo Sura ya 15:1 —

"Baada ya mambo hayo njozi likamjia Abramu katika njozi likanena, usiogope, Abramu, mimi ni ngao yako, na thawabu yako kubwa sana..

1. Abramu akasema, Ee Mungu, utanipa nini na hali sina mtoto, na atakayeimiliki nyumba yangu ni huyu Eliezeri, mdameski?

2. Tazama hukunipa Uzao na mtu aliyezaliwa nyumbani Mwangu ndiye mrithi wangu.

3. Nalo neno la Bwana likamjia likinena, huyu hatakuriithi, bali atakayetoka katika viuno vyako ndiye atakayerithi.

4. Akamleta nje, akasema tazama sasa mbinguini, kazihesabu nyota kama ukiweza kuzihesabu.

Akamwambia, ndivyo utakavyokuwa uzao wako

5. Akamwamini, naye akamhesabia jambo hilo kuwa haki?

Katika maandiko haya, imani ya mteule wa Mwenyezi Mungu Abrahamu inaonekana wazi. Umri wake umekuwa mkubwa zaidi na huenda kama ni enzi hizi za dijitalii na utaalam mwingi wa kisayansi na tiba, tunaweza kusema yeye ni mke wake Sarai walikuwa wamefika umri wa kukataa tamaa ya kujaliwa na mtoto.

Ahadi ya mwenyezi Mungu kwa Abrahamu ni kwamba mbali ni mrithi kutoka kwa viuno vyake (Mwanzo 15:4) , pia uzao wake utabarikiwa kwa idadi kama nyota za angani!

Hapa tunaona kwamba licha ya kuyakabli matatizo Abrahamu anaendelea kuomba na kuchuchumilia yaliyo mbele. Anatupilia mbali dharau, (ama wataka kusema kwamba watu wa siku hizi wameacha kuwadharau na kuwaduni sha wasio na watoto?, Kejeli na kudunishwa.

Ukiwa na lengo maishani ni vyema kulishikilia na kuliandama taratibu huku ukimtegemea Mwenyezi Mungu kwa kulitimiza.

Katika sura ya 17, kitanu cha Mwanzo, kuna videkezo vya muhimu kama ifuatavyo. Kwanza nanukuu maandiko matakatifu yasemavyo:

1. Abramu alipokuwa mtu wa miaka tisini na kenda, Bwana akamtokea akamwambia, mimi ni Mungu Mwenyezi, uende mbele yangu ukawe mkamilifu.

2. Nami nitafanya agano langu katii ya mimi na wewe , name nitakuzidisha sana sana,

3.Abramu akaanguka kifudifudi, Mungu akamwambia akasema.

4.Agano langu nimefanya nawe, nawe utakuwa baba ya mataifa mengi.

Wala jina lako hutaitwa tena Abramu bali jina lako litakuwa baba wa mataifa mengi yaani Abrahamu.

15. Mungu akamwambia Ibrahimu, Sarai mke wako hutamwita Jina lake Sarai, kwa kuwa jina lake litakuwa Sara.

16. Nami nitabariki, na tena nitakupa mwana kwake, naam, nitambariki naye atakuwa mama wa mataifa, na wafalme wa kabila za watu watatoka kwake.

17. Ndipo Ibrahimu akaanguka kifudifudi akacheka, akasema moyoni. Je! Mtu wa umri wa miaka mia kwake atazaliwa mtoto? Naye sara mwenye umri wa miaka tisini atazaa?

Sura hii ina vipengele kadhaa vinavyojitokeza vinavyoweza kusaidia mkristo kufika upeo wa kutimiza sifa ya kuwa na subira maishani.

Kwanza, Mungu anafanya maagano na Abramu na Sarai. Anawataka kubadilika sio tu kwa majina bali na mawazo na desturi yao.

Pili anawahimiza kuweka maagano kati yake na wao kwa kusema, aya ya kwanza ya kwamba.

...Mimi ni Mungu mwenyezi uende mbele yangu ukiwa mkamilifu.

Neno mkamilifu lina maana nyingi, lakini hapa nitasema kuwa ni mtu mwenye nia safi, moyo safi ambaye anatenda mapenzi ya mwenyezi Mungu. Je huyu ni wewe?

Basi endelea kuwa na subira kwani Baraka (heri) inakuja.

Fanya bidii kila saa na kila dakika kuona kuwa unakuwa na uhusiano mwema na Mwenyezi Mungu. Uhusiano huu unapatikana kwa kuwatenda wenzako mema. Pia ni lazima kujitunza ili usimuasi Mungu kwa njia yeyote ile.

Abrahamu na Sarai mke wake walijitahidi sana maishani katika kumfuata Mwenyezi Mungu hata pale walimwengu wenzao walipovutiwa na anasa na tamaa, wao walisalia kutazamia muumba wao.

Je wewe unatazamia nani kuja kuwa mwokozi au mkombozi wako?

https://t.me/magazeti

# Ruto apuzilia mbali wito wa kuvunjwa serikali ya kaunti ya Taita Taveta

NA PASCAL MWANDAMBO

Naibu wa rais William Ruto amepuzilia mbali wito wa kuvunjwa kwa serikali ya Kaunti ya Taita Taveta.

Akihutubia wananchi katika kijiji cha Buguta,kata ya Kasigau, Ruto aliwaonya viongozi kutoka sehemu hiyo kuacha kiburi na kujadiliana jinsi watakavyosuluhisha maswala muhimu yanayohusu kaunti hii.

"Ni jambo la kustaajabisha kuona viongozi kutoka kaunti ya Taita Taveta wakizunguka Nairobi wakitafuta suluhu ya matatizo yanayowakumba kutoka kwa viongozi wa serikali kuu.Kwani hakuna wasomi na viongozi kutoka hapa wenye hekima na maadili ya kuweza kusuluhisha shida zenu?" Makamu wa Rais akauliza.

Ruto alisema kwamba kuvunjwa kwa serikali yoyote ya kaunti si jambo rahisi kwani hata Makueni walijaribu na hilo likashindikana.

"Nataka viongozi wenu wajue kwamba kazi ya serikali kuu si kutekeleza maswala kama vile kuvunja serikali za kaunti bali kutoa huduma za kuboresha maisha ya wananchi na kutekeleza ajenda za maendeleo," akasema Naibu Rais.

Aliwaonya viongozi kwenye kaunti kwamba iwapo wataendelea kushinikiza kuvunjwa kwa serikali ya kaunti, hiyo ingekuwa dalili tosha kwamba wameshindwa na kazi.

"Kama kazi imewashinda mujue kwamba uchaguzi mkuu ujao mtaona kivumbi.Hatuwezi kuvumilia kuona wananchi wakiteseka wakikosa huduma muhimu za serikali huku mkiendelea kuzozana," akasema Ruto.

Yapata miezi miwili iliyopita gavana Samboja aliwashangaza wengi alipotangaza nia ya kuvunja serikali yake na kuanza mchakato wa kukusanya saini za kuhalalisha hilo,baada ya kushindwa kukubaliana na wawakilishi wadi juu ya makadirio ya bajeti.Tayari yadaiwa saini zaidi ya 50,000 zimekusanywa.



Gavana wa Taita Taveta Granton Samboja na Naibu Rais William Ruto.

Hata ingawa wawakilishi wadi wamekuwa wakimsihi Samboja kuketi nao chini ili kuzika tofauti zao, gavana amekuwa ngangari kwamba lazima serikali ivunjwe na uchaguzi kufanywa upya.

Hivi majuzi gavana Samboja aliwatupia cheche za maneno baadhi ya viongozi wa makanisa ambao walimwomba ajiuzulu iwapo ameshindwa kuafikiana na viongozi wengine juu ya swala la makadirio ya bajeti.

Baadhi ya viongozi ambao Samboja alienda kutafuta ushauri juu ya swala hili nyeti ni kinara wa ODM Raila Odinga na Rais Uhuru Kenyatta ambao wako mrengo wa BBI.

Kwa upande wake Ruto na wafuasi wake wanaupinga mrengo wa BBI wakiutaja kama laghai.

Wakati wa mkutano huo ambao gavana Samboja hakuhudhuria, naibu rais alitangaza kwamba serikali imetenga shilingi bilioni 1.2 kwa kaunti ya Taita- Taveta kufadhili miradi ya kueneza umeme mashinani.

Alisema kwamba idadi ya watakaonufaika na mradi huu itafikia watu 20,000 maradufu ikilinganishwa na watu 10,000 wakati serikali ya Jubilee ilichukua uongozi mwaka 2013.

Wakati huo huo,Ruto alitangaza kwamba serikali imetenga zaidi ya shilingi milioni 170 ili kufaidi wasiobahatika katika jamii wakiwemo mayatima,wajane na wakongwe.

"Viongozi wa nyanjani wanatakikana kuhakikisha kwamba kila mlengwa amesajiliwa ili kufaidi kutokana na fedha hizi na pia kuona kwamba pesa hizi hazitofujwa," akaonya Ruto.

# Dalili za saratani ya ulimi na mbinu za matibabu

NAIS`HAQ GUNGA CHEA

Tukiendelea na mazungumzo kuhusu magonjwa ya ulimi, leo tunatoa ufafanuzi zaidi kuhusu saratani za ulimi na mdomoni kwa jumla. Saratani hizi za ulimi hutofautishwa kulinganana sehemu zinakotoka kwenye ulimi na ndani ya mdomo.

Wakati saratani inapojitokeza katika sehemu ya mbele ya ulimi, basi saratani hiyo inaitwa squamous cell kwa lugha ya kimatibabu yaani kiini cha saratani ya sehemu ya ulimi ya kuzungumzia.

Kama saratani hiyo imejitokeza katika sehemu ya nyuma karibu kidogo na shina la ulimi, wataalamu wameipa jina la kiini cha saratani ya chini ya ulimi lakini katika lugha ya kitaalamu saratani hizo zinatumia jina moja la squamous.

Tabia za aina hizi mbili za saratani zinatofautiana pakubwa na zinaashiria tofauti ya asili za magonjwa hayo. Kwa sababu ya kuwa na asili tofauti kati ya magonjwa hayo mawili, basi hata taratibu za matibabu kadhalika ziko tofauti, yaani hazifanani.

Kwa kawaida saratani za ndani ya mdomo ni chache ikilinganishwa na aina nyingine za saratani, na zinawakilisha asilimia tatu tu ya aina za saratani zilizopo.

Kidesturi dalili za ugonjwa huu wa saratani ya ulimini ni kujipata na kidonda kando kando ya ulimi cha rangi nyekundu iliyochanganya na pink, vidonda ambavyo hukaa kwa muda mrefu visivyoonekana kupona.

Vidonda hivi huanza kutokwa na damu kwa urahisi vinapoumwa kwa meno au vinapoguswa. Itakapokupata hali hii hakikisha unakwenda kutafuta ushauri wa daktari, hasa kama mwenye kuugua anapata umri wa miaka hamsini na zaidi.

Katika siku za kwanza za ugonjwa huu wa saratani ya sehemu ya chini ya ulimi, huwa hautokei na dalili zinazoweza kuonekana wazi wazi. Hii ina maana ya kwamba ugonjwa huu haujitokezi mapema ukajulikana hadi baadaye.

Hata hivyo dalili zinaweza kudhihiri kwa kuhisi maumivu kwenye ulimi na sehemu nyingine ndani ya mdomo. Dalili nyengine ni sauti kubadilika, matatizo ya kumiza, kutojisikia timamu.

Kwa kuwa dalili za kwanza za ugonjwa huwa hazipo, saratani nyingi za aina hii zinazotokeza chini ya ulimi, huwa zimepevuka wakati unapokwenda kumwona daktari. Wengi wa wagonjwa watakuwa wamefanya uvimbe kama chunusi kwenye eneo la ndani ya shingo.

**Sababu sa magonjwa**

Kwa hakika magonjwa haya ya saratani ya ulimi hayajagunduliwa asili yake, bali wataalamu wanasema ukosefu wa kuuweka mdomo katika hali nzuri ya usafi, na kuwa na mabaka meupe mazito kwenye ngozi nyembamba inayofunika sehemu za ndani



ya mdomo huenda ikawa ndizo sababu.

Sababu nyingine zinazotajwa ni kuwepo na hitilafu katika ini, kaswende, ulevi wa kupindukia na kuvuta sigara kupita kiasi.

**Walioathirika zaidi**

Ugonjwa wa saratani ya ulimi imewaathiri wanaume wa zaidi ya umri wa miaka sitini. Ugonjwa huu ni mchache miongoni mwa watu wa chini ya umri wa miaka arobaini, hasa wanawake.

Ugonjwa mwingine wa saratani unajulikana kama Carcinoma, ambao hushika sehemu za mashavu ambapo hutokea uvimbe unaoweza kuuhisi kwa ulimi. Uvimbe huo huandamana na maumivu ambayo hukufanya ukapata matatizo ya kumeza vitu, mishipa ya mashavu kuwa migumu na kutokwa na damu.

Ugonjwa huu unaweza kusambaa hadi kwenye ngai za shingoni zenye kuzalisha mate. Njia bora zaidi ya kuugundua ugonjwa huu ni kwa mtaalam aliyebobea kuchukua sehemu ya vinyama vya shavu katika eneo lililopata ugonjwa, na kuvifanyia uchunguzi.

Mhusika atafanyiwa uchunguzi wa kujua mahali halisi uliposhika ugonjwa huo na hali ugonjwa huo ulipofikia, kwa utumiwaji wa vifaa vya MRI au CAT. Kwa kufanya hivyo daktari atafahamu mbinu atakazotumia kukabiliana na ugonjwa huo, na kwa kipindi gani atakachotumia katika matibabu kulingana na jinsi mgonjwa atakavyokuwa akirudi kwa daktari kupata matibabu.

**Aina ya matibabu**

Sio wataalamu wote wa matibabu wanakubaliana juu ya aina ya matibabu ya saratani ya ulimi na mdomo kwa jumla. Hata hivyo wengi wao wanakubali kwamba kama kuna mahitaji yoyote ya huduma za usafi wa mdomo kwa jumla, taratibu hizo zinapaswa kufanywa kabla ya matibabu ya saratani kuanza, na kama mhusika anavuta sigara itamlazimu kuacha.

Matibabu yataanza kwa upasuaji na kisha kufuatiwa na huduma ya radiation yaani matibabu ya kutumia nguvu na mwangaza usioonekana.

https://t.me/magazeti


THE DOWN LOWS AND UP HIGHS ON EVERYTHING
ENTERTAINMENT!




Be sure to grab your free copy today!
pulser
Get your magazine online on
www.pulser.co.ke/magazine

DARASA LA **FASIHI**

# Dhana na siri katika hadithi fupi ya 'Tulipokutana Tena'




**Kitabu:** Tumbo Lisiloshiba
**Hadithi:** Nizikeni Papa Hapa
**Mwandishi:** Ken Walibora
**Chapa:** Longhorn Publishers (K) Ltd

**NA MWALIMU PAMBAZUKO**

Mwandishi wa hadithi hiyo iliyo katika mkusanyiko wa 'Tumbo lisiloshiba na hadithi zinginezo' anaeleza changamoto za maisha walopitia wahusika wake wakuu hususan Bogoa.

Hadithi inaeleza kuhusu mazungumzo ya wahusika wanne.Mazungumzo haya katika hoteli ya Rombeko jijini Seka.

Katika mazungumzo hayo swala la dhana ya uchawi lilichipuka huku mmoja wa wahusika akidhania kabila la wenzake hushiriki katika mambo ya uchawi.

'Nyinyi wamate si hamuhitaji ndege mnapotoka safari au siyo? Mnaruka tu hewani kama ndege mkitumia uchawi wenu!' Kazu alieleza suala kwa Sebu muhusika mkuu (uk.104)

Hii ni dhana ya kudhania kabila Fulani ina ila bila kujua ukweli wake.Dhana hukua nakuonekana kama kweli ikiwa inaaminiwa.

Dhana ni kitu ambacho hakina uhakika kama ni kweli ama uwongo (allegation). Kazu alozua dhana hiyo anakumbushwa kuwa hadithi za kichawi ziko kila pahala duniani.

Dhana hii ya uchawi kwa mfano imekuwa pia miongoni mwa wakenya ambao huona kabila ama jamii fulani huwa na ila ama kasoro fulani.

Utasikia wakisema 'lo! Wakikuyu ni wezi, ama 'wapwani hufuga majini', 'wakamba ni wazinifu' na kadhalika.

Ukweli ni kuwa katika kila jamii kuna ila mbalimbali na huwezi kuchukua kisa ama visa fulani kujumuisha jamii nzima.

Kuna wezi miongoni mwa makabila mengine mbali na wakikuyu wanaodhaniwa hivyo.Karibu makabila yote yana visa vya kichawi na si wapwani pekee.

Miongoni mwa jamii kuna wabaya na wazuri.Kuna wachawi na wezi wakichina,kizungu,kihindi na kiafrika ilivyo umasikini, utajiri na ucha mungu.

Katika muktadha huu visa hutolewa kuashiria uchawi wa jamii fulani kwa mfano habari ya kupiga mateke mapakacha sehemu ya Mate.

'nasikia ukitembea usiku huko na ukitokezea kuliona pakacha usilipige teke. Ukilipiga hiari yako.Mara utasikia likikuambia ,bwana we, huoni kwamba unaniumiza? Katafute mpira uupige shuti, mimi ni binadamu mwenzako!' (uk.105)

Sebu anawambia wenzake kuwa uchawi ni sayansi na kuwa hata wazungu wanaamini uchawi uko ijapkuwa mara nyingi hakuna ushahidi wazi wa kuweko kwake.

Uchawi hapa unaitwa sayansi kwa sababu inahusisha vitu ambavyo havijulikani kwa mwanadamu ilivyo sayansi tunayoielewa ambapo kila uchao uvumbuzi mpya hufanywa.

Tunaelezwa jinsi mtu anavyoweza kurushwa kutokea sehemu moja hadi nyingine na kupotea bila kuonekana kupitia sayansi hii ya uchawi.

Kwa muktadha huu muhusika mkuu anasimulia jinsi rafiki yake wa utotoni kwa jina Bogoa alipoletwa kijijini na wazazi wake maskini ili kulelewa.

Tunaelezwa kuwa ghafla Bogoa alitoweka kijijini mule akiwa na miaka 19 mwaka 1966 na hakuna aliyepata kumuona tena hata alipotoka ambapo wazazi wake walifariki.

Kwa bahati nzuri Kazu alimkumbuka huyo Bogoa na kumueleza Sebu kuwa alifanya kazi kama sonara sehemu ya Tinya alipoowa na kupata watoto na kuwa anafahamu aliko.

Baadae huyo Bogoa ambaye jina la pili ni Bakari aliweza kukutana na rafiki wake wa zama muhusika mkuu Sebu baada ya kujulishwa na Kazu.

Sebu akiwa na mkewe Tunu aliweza kukutana na Bogoa katika kilabu cha Pogopogo.Kazu na mkewe Temu pia walikuwa hapo.

Kukutana kwa marafiki hao wa kale kulileta furaha kubwa jinsi walivyokumbatiana kama smaku.Bogoa akiwa na mkewe Sakina walifurahi kwa mapatano yale.

Hali hii ilidhihiri kuwa urafiki wakati mwengine hushinda ndugu na milima haipatani lakini wanadaamu hukutana.

Katika mazungumzo yao ya kumbukumbu Bogoa alitoboa siri aloificha moyoni kwa miaka mingi na ambayo hata mkewe Sakina hakuijua.

Anasema kuwa wazazi wake walimuhadaa na kwa sababu ya shida na kumuacha kwa Bi.Sinai ili apate malezi hapo.

Bogoa anaeleza mateso makubwa aloyapata hapo kijiji cha Seka.Alifanywa kama tambara bovu huku akifanya kila aina ya kazi ya nyumbani.Anasimulia:-

'Kumenyea Bi Sinai , bibiye wa nyumba hiyo vitunguu maji, vitunguu thomu, na malimau,kumkunia nazi,kumparia na kumtolea matumbo samaki,kumkatia shiago za nyama...' (uk.115)

Bogoa aeleza hakupelekwa shule wala kuruhusiwa kucheza na watoto wenzake bali watoto wa jirani kama Sebu .

Sebu hakufikiria kuwa Bogoa wakati ule alikuwa akiteseka na akamuuliza kwanini hakumwambia yalomkumba?

Bogoa alimjibu kuwa Bi. Sinai alimuonya asiseme mateso yale na hata wazazi wake waliopofika kwa mara mwisho kumuona hakupewa nafasi ya kutoboa mateso alokuwa anapitia.

Siri hii ilimshangaza sana Sebu na kumsikitisha lakini ni baada ya kukutana tena na rafiki yake wa utotoni.

https://t.me/magazeti

Kiswahili **KITUKUZWE**

## Sentensi ni kipashio cha juu zaidi katika tungo

**NA FADHILA HAMISI**

**SENTENSI**
**Maana:**
Sentensi ni kipashio cha juu zaidi katika tungo chenye muundo wa kiima na kiarifu ambacho hutoa taarifa kamili.

**AINA ZA SENTENSI**
**1. Sentensi Sahili/huru**
Hizi ni sentensi ambazo huundwa kwa kishazi huru kimoja ambacho hutoa taarifa kamili Kishazi huru hicho kinaweza kuundwa na kitenzi kikuu peke yake.
Mifano katika Sentensi
I.Sakina anaoga bafuni.
II.Nyanya anafagia uwanjani pake.
III.Mwalimu mkuu hakuwa anataka kutia sahihi barua ya mwaliko wa wanafunzi wake kuhudhuria kongamano hilo.
IV.Kiatu ki mezani.
V.Yeye ndiye aliyekula ndizi.
VI.Sisi ndisi tuliowaalika watoto hawa katika sherehe hizi.
VII.Mwalimu Yeya alikuwa anataka kwenda kupumzika nilipowasili.
VIII.Kalamu I dawatini mwangu.
IX.Mayai ya chumbani kwa babu.
X.Walikuwa wakirushiana cheche za matusi tulipowakaribia.

**2. Sentensi changamano**
Hizi ni sentensi ambazo huundwa kwa kishazi tegemezi na kishazi huru.
**Mifano katika Sentensi**
I. Viti vilivyonunuliwa jana vitapelekwa kijijini.
II. Kitabu kilichoipotea kilikuwa cha mwalimu Nzili.
III. Samaki waliovuliwa leo ni wakubwa mno.
IV. Nguo zilizoletwa jana zinapelekewa watoto yatima. V. Uzi ulioshonewa nguo hii umeoza.
VI. Chakula kilichopikwa na dada ni kitamu sana.
VII. Wageni watakaowasili kesho watalala nyumbani kwa kaka.
VIII. Peremende zilizonunuliwa na babu ni za wajukuu wote wa hapa.
IX. Milango iliyopakwa rangi leo inapendeza sana.
X. Wanafunzi waliofeli katika mtihani wao wa mwisho wa muhula watarudia.

**3. Sentensi Ambatano**
Hizi ni sentensi ambazo huundwa kwa vishazi viwili au zaidi pamoja na kiunganishi.
**Mifano katika Sentensi**
I. Mwalimu anafunza na wanafunzi wanaandika wakimsikiza.
II. Watoto walikua vizuri ingawa walilelewa katika mazingira duni.
III. Maji yaliyoletwa yana chumvi ilhali yametoka kisima cha maji baridi.
IV. Wanafunzi waliopotea wamepatikana na vifaa viliyoibwa vimeregeshwa.
V. Wachezaji hao walishangiliwa sana licha ya wao kishindwa.
VI. Mpishi aliyekiandaa chakula hakupata fursa ya kukila lakini wageni wote waliowasili walikula.
VII. Maji yanayotoka kwenye mfereji yatakatwa endapo bima ya eneo hili haitalipwa kufikia jioni.
VIII. Wavuvi wataambulia hasara kwa sababu ya ukosefu wa umeme katika sehemu zao za kuhifadhia samaki.
IX. Kiranja alimwadhibu Karanja kwa kuwa alimuona akicheza mpira wakati wa vipindi vya masomo.
X. Sakina alifeli katika mtihani wake wa kitaifa licha ya kusoma kwa bidiii na kuwa makini darasani.

CHEMSHA **BONGO**




Septemba 18 - 24 | Pambazuko

# Mitihani



## SOCIAL STUDIES




**RAPENDA AREA**

**1. The approximate length of the railway line shown on the map is**

A. 12km
B. 11km
C. 10km
D. 9km

**2. The general direction of flow of River Rapenda is**

A. South West to North East
B. South East to North West
C. North West to South East
D. North East to South West

**3. A trader in Rapenda town can obtain a trading license from the**

A. post office
B. County office
C. District office
D. police station

**4. The following activities are carried out in Rapenda area except**

A. Fishing
B. farming
C. Mining
D. Trading

**5. The main natural vegetation in the southern part of Rapenda area is**

A. Forest
B. Scattered trees
C. papyrus swamp
D. scrub

**6. The main source of water for Rapenda town is a**

A. dam
B. river
C. borehole
D. Swamp

**7. The highest point in Rapenda area is**

A. Nazu zone
B. Bura zone
C. Ture zone
D. Naru zone

**8. Which one of the following is a responsibility of children in a family?**

A. sharing out family resources
B. respecting adults
C. ensuring family protection
D. building of family confidence

**9. Lake Victoria was formed as aresult of**

A. folding
B. human activity
C. vulcanicity
D. down warping

**10. Three of the following statements are true about the importance of the institution of marriage. Which one is not?**

A. it ensures continuity of the society
B. it prevents contracting of HIV and AIDS
C. it provides companionship
D. it brings unity among people

**11. Which one of the following African countries was the last to attain independence?**

A. Ghana
B. Zimbambwe
C. Tanzania
D. Kenya

**12. Which was the best means of communication to use to send message to distance places in the past?**

A. drum beating
B. ululation
C. fire signals
D. messengers on foot

**13. In Kenya external enemies are prevented from entry by**

A. national youth service
B. kenya defense forces
C. prisons department
D. national police

**14. In traditional Kenyan societies initiation was important because**

A. it marked the end of childhood
B. it prepared the youth for future adult roles
C. it promoted young men to warriors
D. it helped youth to be warriors

**15. Which one of the following factors influence the climate of a place?**

A. high population
B. permanent rivers
C. food crops
D. prevailing winds

**16. Which country is CORRECTLY matched with its capital city?**

| | Country | Capital city |
|---|---|---|
| A | South Sudan | Khartoum |
| B | Gambia | Banjul |
| C | Libya | Tunis |
| D | Zambia | Harare |

**17. the Nandi rebellion in Kenya was led by**

A. lenana B. Mukite
C. Kimyole D. Samoei

**18. Which one of the following is the MAIN benefit of horticultural farming in Kenya?**

A. it is a source of vegetables
B. it is a source of foreign exchange to the coutry
C. it has created employment opportunity
D. it is a source of income to the farmers

**19. Which one of the following countries in Africa is not a member of COMESA?**

A. Malawi B. Ethiopia
C. Tanzania D. Uganda

**20. The MAIN problem facing pastoral communities in Kenya is**

A. inadequate market B. cattle rustling
C. attack by tsetse flies D. drought

**21. The main source of revenue for the National government in Kenya is**

A. income tax
B. loan
C. grants
D. excise duty

**22. The reasom why the floor of Rift valley is always dry is that**

A. the area is below the sea level
B. it is rocky
C. it has many salty lakes
D. it lies between the Eastern and Western highlands

**23. Which one of the following courts in Kenya is the lowest?**

A. Chief magistrate court
B. court of appeal
C. supreme court
D. high court

**24. The following are characteristics of a relief region in Kenya**

i) it is generally dry
ii) it has hills that resisted erison called inselbergs
it lies between 600-1500m above the sea level

the relief region described is;

A. The Rift valley
B. The lake basin
C. the highlands
D. The nyika plateau

**Study the map below and answer questions 25-28**



**25. The reason why river projects were established on the river marked D was to;**

A. promote industrial development
B. provide water for irrigation
C. attract tourists
D. control floods

**26. Road transport is less developed in the area marked XXX mainly because**

A. the region receives low rainfall
B. the region is affected by insecurity
C. the relief of the region is hilly
D. the region is sparsely populated

**27. There is little trade between kenya and the country marked Y mainaly because of**

A. production of similar goods
B. poor road network
C. language barrier
D. political instability

**28. Deforestation is discouraged in the shaded region marked G because**

A. trees help lower the temperatures of the region
B. the government wants to conserve indigenous species

https://t.me/magazeti



C. trees protect water towers

D. trees protect wildlife

**29. Which one of the following factors mainly determines the location of a cement manufacturing industry?**

A. nearness to raw materials

B. nearness to market

C. availability of transport

D. availability of labour

**30. Which one of the following is not a contribution of minerals to the economy of Kenya?**

A. provides employment

B. lead to growth of towns

C. leads to growth of slums

D. leads to provision of good transport and communication

**31. Which one of the followi9ng groups share a common ancestor?**

A. grandfather, father, son

B. brother, sister, grandmother

C. grandfather, mother, son

D. father, mother, grandfather

**32. Which one of the following methods is true to mine soda ash in lake Magadi in kenya?**

A. deep shaft method

B. evaporation

C. dredging

D. open cast

**33. Which statement is true about traditional education in the pre-colonial period?**

A. learning took place in special places

B. learning took place throughout ones life

C. learning started immediately after initiation

D. educating the young was the responsibility of the clan elders only

**34. Which none of the following Africa traditional societies lived in small group of families before the coming of the Europeans?**

A. the san B. the khoikhoi

C. Abawaga D. Soninke

**35. Rural- unban migration can Best be managed by;**

A. improving transport in rural areas

B. establishing industries in rural areas

C. giving the needy in rural areas financial help

D. establishing market places in the rural areas

**36. Which one of the following industries in kenya is correctly matched with its products?**

| Type of industry | product |
|---|---|
| A. manufacturing | bicycles |
| B. service | textile |
| C. processing | sugar |
| D. assembly | publishing |

**37. Below are statements of an organization in Africa**

I) it was formed in 1976

ii) it provided common services to member countries

iii) it collapsed in 1977

the organization described above is


A. the Organization of African Union (OAU)

B. The East African Community (EAC)

C. The Preferential Trade Area (PTA)

D. The Common Market for East and Central Africa (COMESA)

**38. The diagram below shows sections of a slope marked A,B,C and D**




In which part of the slope would soil erosion be least destructive

A. C B. D C. B D. A

**39. Which one of the following is true about tourism in Kenya?**

A. it is the leading foreign exchange earners

B. it enhances development of moral values

C. most of the tourists come from Asia

D. the main tourist attraction is winter sports

**40. Which one of the following is a cause of conflict in society**

A. partnership in elections B. difference in opinion

C. cultural differences D. scarcity of resources

41. Who among the following African leaders was a founder member of Kenya African National Union (KANU?

A. Daniel Moi B. Ronald Ngala

C. James Gichuru D. Paul Ngei

**42. Below are statements describing some activities of the early human beings. They**

i) made simple stone tools

ii) use gestures to communicate

C. ate raw food

D. lived in small groups

Which one of the following early human beings are associated with the above activities?

A. Homo Sapien Sapiens

B. Homo erectus

C. Homo Habilis

D. Homo Sapiens

**43. A driver noticed the road sign drawn below on a highway. The best action for him to take was**



A. stop immediately

B. drive slowly

C. get out of the vehicle

D. call the police

**44. Three of the following are powers of the president of Kenya. Which one is not?**

A. declaring a seat vacant in parliament

B. declaring a state of emergency with approval of the national assembly

C. appointing the attorney general with the approval of the national assembly

D. pardoning petty offenders

**45. Which of the following climatic regions is represented ion the bar graph?**

A. savanah climate B. equatorial climate

C. semi-desert climate D. Mediterranean climate

**46. Which one of the following statements is true about Leopold Sengor and Nelson Mandela**

A. a lot of development was realized during their leadership

B. the formed political parties that led their countries to independence

C. both were founders of OAU

D. they formed and mobilized military to fight the colonial government

**47. Three of the following are results of the coming of the missionaries inti East Africa. Which one is not?**

A. establishment of schools and formal education

B. conversion of Africans to Christianity

C. promotion of African culture

D. opening up of churches and hospitals in the interior

**48. The diagram below shows a feature formed by a river as it approaches its mouth. Which of the following lakes was formed in this manner?**

A. Lake Shaba

B. Lake Chad

C. Lake Edward

D. Lake Kanyaboli

**49.The time at Conakry in Guinea is 10.00am at 140W. what is the time at Tunis in Tunisia at 100E?**

A. 11.36pm B. 9.24pm

C. 9.24am D. 11.36am

**50. As Kamau walked home from school one evening he saw a man knocked down by a moving vehicle. The best action for Kamau to take was**

A. go home and call his parents to come and help

B. administer first aid

C. leave the man alone

D. report the matter to a police station

**51. The Akosombo dam in Ghana was constructed mainly to;**

A. provide water for irrigation

B. produce hydro-electric power

C. control the floods

D. reduce cost of generating electricity from oil

**52. School rules and regulations are used mainly to**

A. encourage students to excel in their studies

B. identify forms of misbehavior among students

C. protect weak students from harassment by others

D. to promote discipline within the school

**53. in which section or chapters of the constitution of Kenya are rights and freedoms of individuals stated?**

A. The executive / chapter 9

B. bill of rights/ chapter 4

C. citizenship / chapter 3

D. application of constitutional rights / art 52-57

**54. The following are varieties of coffee grown in both Kenya and Ethiopia**

i) Arabica

ii) Robusta

which of the following describes the aArabica coffee?

A. it is grown in the highlands

B. it fetches lower prices than Robusta

C. It does well in the lowlands

D. it is favoured by hot and wet conditions

**55. The main function of the legislature is to make and amend laws. At what stage does the third reading take place during the law making process?**

A. 1st stage B. 4th stage

C. 3rd stage D. 5th stage

**56. The main reason behind the Berlin conference in 1884-1885 in Germay was**

A. to organize the scramble of Africa

B. to organize the participation of Africa

C. the organize how the colonial powers could rule Europe

D. to look for raw materials in Africa

**57. Parliamentary debates in Kenya's national assembly are chaired by:**

A. the attorney general

B. the president

C. the speaker

D. the clerk of the national assembly

**58. The last census in Kenya was done mainly to**

A. enable the government to plan for its citizens

B. arrive at the population density of Kenya

C. enable the government to know the wealth of its people

D. enable the government to plan for elections

59. The chairperson of the independent Electoral and Boundaries Commisson is appointed by the

A. judiciary B. national assembly

C. attorney general D. head of state with the approval of national assembly

**60. Steve has poor eyesight. He is not allowed to play with his age mates by his parents. Which one of the flowing freedom is Steve denied?**

A. expression B. worship

C. association D. movement

https://t.me/magazeti

## MAJIBU KISWAHILI SEPTEMBA 11-17

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | B | 11. | A | 21. | A | 31. | C | 41. | C |
| 2. | B | 12. | B | 22. | B | 32. | B | 42. | A |
| 3. | A | 13. | A | 23. | D | 33. | B | 43. | D |
| 4. | D | 14. | B | 24. | D | 34. | D | 44. | C |
| 5. | A | 15. | D | 25. | B | 35. | B | 45. | |
| 6. | A | 16. | A | 26. | D | 36. | C | 46. | A |
| 7. | C | 17. | C | 27. | B | 37. | A | 47. | D |
| 8. | B | 18. | C | 28. | A | 38. | C | 48. | A |
| 9. | B | 19. | C | 29. | C | 39. | A | 49. | C |
| 10. | B | 20. | B | 30. | C | 40. | A | 50. | A |

# Umuhimu wa funga ya Ashura katika dini



Asalam aleikum warahmatullahi wabarakatu. Kwa jina la Mwenyezi Mungu Allah mwenye kuneemesha neema ndogo kwa kubwa.

Tukiwa katika mwaka mpya ya Kislamu ndani ya mwezi wa kwanza wa Muharaam tutaangazia umuimu wake hususan katika siku ya 9 inayoambatana na sikukuu ama funga ya siku ya Ashura.

Ashura ni siku nyeti kabisa katika kalenda ya kiislamu. Ni siku ya kukumbuka kufaulu kwa Nabii Musa (AS) dhidi ya kafiri firauni mtawala muovu wa Misri.

Ashura inatukumbusha kisa kizito cha Nabii Musa (AS) alowanusuru bani Israeli (wana wa Israeli) toka kwa utumwa wa firauni.

Kisa hichi cha Nabii Musa (AS) kimeelezwa katika Quran takatifu. Ingawa walohusishwa ni bani Israeli lakini ni mfano tu kwa wanadamu wote.

Katika kisa hicho cha Nabii Musa (AS) twaelezwa jinsi mamake alivyomuweka kikapuni ili amuokowe kupitia mtoni kutoka kwa Firauni aliyekuwa anawaua watoto wa kiume.

Aghalabu kwa nguvu na uwezo wa Allah Azzah Wajallah kitoto kile kilinusurika na hata kulelewa na mke wa firauni.

Twaelezwa miujiza ya Allah (SWT) aliyompa Musa (AS) ili apambane na firauni aliyetakabari na hata kujiita mungu.

Firauni alitaka kujaribu nguvu za Mungu wa Musa (AS) na akaona lakini akawa sugu wa kuamini. Musa alipoonyesha miujiza ya fimbo kugeuka nyoka firauni naye akawaleta wachawi wake wakafanya hivyo hivyo.

Quran yaeleza katika sura ya 20 yaani Taha hivi. "(Kwa Musa)...tupa bakora yako chini itavimeza walivyobuni kwa mazingaombwe hawatafaulu (Taha 20; 67-69).

Hapo vile vijoka vya wachawi na waganga wa firauni vikamezwa vyote na joka kuu la Musa (AS). Kwa mshangao huu twaelezwa kuwa wale washirikina ama wachawi wote walimsujudia Allah (SWT) wakisema:

"Twaaamini Mungu wa Musa na Harun kuwa ni wa kweli." (Taha 20: 70).

Hatimaye kuona ameshindwa firauni alishikwa na hasira na kutaka kumuangamiza Musa (AS) ambaye aliongoza msafara wa watu wake bani Israeli kutoka Misri kwenda ng'ambo ya pili.

Msafara wa Musa (AS) ulifika ukingoni pwani ya bahari wasijuwe watapitia wapi huku maadui firauni na jeshi lake wakiwafata unyo unyo.

Akiwa na imani kwa Mola wake Quran katika sura ya Ash-Shu'arah sura ya 26 aya ya 62 inamnukuu Musa (AS) akisema:

"...sina hofu. Mimi niko na Mungu. Atanilinda (kuniongoza)."

Sambamba na maelezo ya kisa hicho Allah (SWT) asema katika sura ya sita Al-An'am aya ya 63 hivi:

"Kisha tukamuwezesha Musa: Piga bahari kwa kifaa hicho na bahari itatawanyika mara mbili na kila upande uwe mfano wa minara miwili mirefu ya milima." (Al-An'am 6:63).

Na hivyo ndivyo ilivyokuwa na msafara wa Musa (AS) kutembea nchi kavu katikati ya bahari ilojitenganisha kuacha njia hiyo kavu.

Firauni na jeshi lake walivyoona miujiza ile ya Allah (SWT) eti nao wakajisopeka kuwafata katika njia ile kavu. Waliangamia wote bahari ilipowazowa!

Kisa hichi kizito ndicho kiini cha waislamu kufunga siku hii ya kukumbuka. Tujuavyo mitume wote ni wa imani moja na Uislamu umeweka hilo wazi ndipo visa vya mitume vyote hupatikana katika Quran.

Siku moja Mtume Muhammad (SAW) aliwakuta mayahudi (bani Israeli) wakifunga akawauliza ni kwa sababu gani. Walimjibu ni kukumbuka siku ya kuokolewa kwao na Nabii Musa (AS) kutoka kwa udhalimu wa firauni kwa miujiza ya Mungu.

Mtume (SAW) aliwajibu kuwa kwa waislamu wana haki kubwa ya kuadhimisha siku hiyo kuliko wao kwani Nabii Musa anahusiana na imani ya Kiislamu halisi.

Ni wakati Mtume (SAW) alipoanzisha funga hii ya Ashura. Twaelezwa na Mtume (SAW) kuwa atakayefunga siku hii basi madhambi yake ya mwaka ulotangulia hufutwa.

Ni jambo la muhimu sana kujifunza kwa kisa kizima cha Nabii Musa (AS). Je, tunajifunza mambo gani na tunayatekeleza kivipi duniani.

Kwanza tunajifunza kuwa na imani kwa Mwenyezi Mungu aliye Muweza kwa wote. Tunaona jinsi gani Musa (AS) alivyokuwa na imani illiyofanikisha ushindi dhidi ya firauni.

Imani yake ilimnusuru na kuweza kuwanusuru watu wake toka kwa firauni kwa kupita katika njia ilowekwa baharini kwa miujiza ya Allah (SWT).

Twajifunza kuwa nguvu za mwanadamu haziwezi za Allah (SWT) kwani mazingaombwe au uchawi wa mwanadamu si kitu kwa Allah (SWT).

Twajifunza kuwa na subra wakati wa changamoto za maisha huku tukimuomba Allah(SWT) atunusuru kwani ndiye kinga yetu jinsi alivyomnusuru Musa (AS) na watu wake.

https://t.me/magazeti

## ULIZA UJIBIWE NA MAALIM THABIT

**SWALI: Je, kuvuta sigara ni haramu ama makuruu? Mchinga wa Machingaa, +255723968181, Tandale Dar-es-Salaam, TZ**

**JIBU:** Chochote kinachodhuru afya yako ni haramu. Naam kwa muktadha huo sigara ni haramu.



**SWALI: Kuna shekhe wetu wa msikiti wa Garissa asema mairungi haina ubaya na pia hutafuna kwa fujo. Je, tukubaliane naye na. Je, afaa kufatwa kama Imamu? Abdille Jama, SMS Garissa**

**JIBU:** Mairungi ama Miraa ni ulevi hivyo ni haramu. Jamaa huyo hafai kuwa imamu ni mfano mbaya kwa waumini na haswa vijana anaoongoza.

**SWALI: Je, kama waswali na hujui kuswali swala zako zitakubalika? Sofia Seif, Mombasa +254758289673.**

**JIBU:** Naam zitakubalika mradi uwe na nia.Hatahivyo ni muhimu kujifunza kuswali.Aidha daima swali nyuma ya imamu haswa katika swala ya jamaa. Kuna vitabu vingi vya mafunzo ya swala nunua pia katika mitandao kuna mafunzo hayo na pia CD ama pia jifunze madrassa ama kwa imamu.



**SWALI: Je. Hadith Qudsi zina umuhimu gani kwa maisha ya muislamu? Salim Moto, Koru-Muhoroni +254712933067**

**JIBU:** Hadith Qudsi na maelezo ama amri za Allah (SWT) yalotamkwa na Mtume Muhammad (SAW). Hivyo ni kama Quran ni lazima kutekeleza katika maisha vyenginevyo utakuwa unaenda kinyume na amri za Mola wako na utakuwa hasarani.

**SWALI: Nashindwa kuelewa maulid ni faradhi ama sunnah na aliyeanzisha ni nani? Ibrahim Dalato, Simba Dishes, Malindi +254729669585**

**JIBU:** Si faradhi au Sunnah.Hatahivyo, hatuwezi kuwahukumu kimakosa wanaotekeleza maulidi kwani ni wasifa wa Mtume Muhammad (SAW). Historia yaeleza maulid yalianzishwa na utawala wa kiislamu wa Fatimiyyah karne ya 600 kule Misri.

Wanaounga mkono maulid wanadai ni muhimu kumpenda kwa kumsifu mtume taib na wanaopinga hudai ni uzushi(bid'ah) Mtume hakufanya. Siungi mkono ama kulaumu upande wowote kwani ni swala la hitilafu. Allahu yaalam.

**TUMA SWALI LAKO LA DINI KWA AIDHA BARUA PEPE : thabiti1964@gmail.com AMA SIMU +254723068181. HAKIKISHA UMEANDIKA JINA KAMILI NA MJI UNAOTOKA. ASANTE.**



Mwanasoka wa timu ya wanawake wa Thika Queens akipambana na mpinzani wake katika kinyang'anyiro cha ligi kuu ya wanawake nchini iliyopepetwa uwanja wa Thika.

# Thika Queens wafanya vyema katika ligi kuu ya Wanawake

**NA ANTHONY AROSHEE**

Thika Queens FC walifanikiwa kujizolea jumla ya alama sita baada ya kushinda mechi mbili za ligi kuu ya Soka ya Wanawake nchini WPL dhidi ya timu za Trans Nzoia Falcons FC na Zetech Sparks FC zilizochezwa mwishoni mwa juma lililopita.

Nahodha Fauzia Omar na mshambuliaji hatari wa timu ya taifa ya Wanawake ya Harambee Starlets Mwanahalima 'Dogo' Adam waliiongoza vyema Thika Queens katika harakati zao kwa kufunga mabao mawili kila mmoja kwenye ushindi wao mabao 6-2 dhidi ya wageni wao timu ya Trans Nzoia Falcons katika mchezo uliofanyika Thika Stadium Jumamosi iliyopita.

Omar alifunga mabao yake katika dakika ya 17 na 47 ilhali Mwanahalima alipachika mabao mawili wavuni dakika ya 56 na 66 huku mabao mengine mawili ya Thika Queens yakifungwa na Lucy Ikhumba dakika ya 33 na Salome Akoth kunako dakika ya 80.

Nayo mabao ya Trans Nzoia Falcons yalifungwa na Irene Khasanti dakika ya 61 pamoja na Martha Amunyolete dakika ya 81.

Katika mechi ya pili, mabingwa hao wa ligi kuu ya wanawake nchini mwaka 2016 Thika Queens waliwacharaza wenyeji wao Zetech Sparks mabao 4-0 kwenye Uwanja wa Ruiru, siku ya Jumapili iliyopita.

Hatahivyo, Trans Nzoia Falcons walimalizia hasira zao za kufungwa vibaya na Thika Queens walipolipiza kisasi kwa kuwanyeshea Makolanders Ladies FC mvua ya mabao 7-2 katika mechi iliyofanyika Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Camp Toyoyo ulioko jijini Nairobi.

Mchezaji Tumaini Waliaula aliwafungia Trans Nzoia Falcons mabao matatu pekee yake katika dakika ya 32, 70 na 85 huku mabao mengine yakifungwa na Irene Khasanti dakika ya 63 na Millicent Ayuma katika dakika ya 83. Naye Martha Amunyolete ndiye aliyewafungia Trans Nzoia Falcons mabao mengine mawili kunako dakika ya 84 na 86.

Mabao ya Makolanders Ladies yalipachikwa kimyani na Lonya Any dakika ya 74 na Shann Adhiambo katika dakika ya 76.

Nao Vihiga Queens FC waliwatandika Wadadia FC mabao 5-0 katika uwanja wa Mumias Sports Complex huku bao la kwanza likifungwa na Terry Engesha dakika ya 22 kabla ya Topister Situma kuongeza bao lam pili dakika moja baadae kabla ya timu hizo kwenda mapumzikoni.

Katika kipindi cha pili, Cynthia Shilwatso aliongeza idadi ya mabao kwa kufunga mabao mawili katika dakika ya 47 na 79 kabla ya Topister kuhitimisha ushindi huo kwa kufunga bao la tano na la ushindi katika dakika za nyongeza, likiwa ni bao lake la pili kwenye mechi hiyo.

Kuhusu matokeo ya mechi nyingine zilizochezwa Jumamosi iliyopita, Gaspo Women walipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wageni Mathare United Women katika Uwanja wa Ruiru wakati Eldoret Falcons FC kutoka Kaunti ya Uasin Gishu walilazimishwa kutoa sare ya 0-0 nyumbani na timu ya Kibera Girls Soccer Academy ya Nairobi kwenye Uwanja wa Eldoret University.

Oserian Ladies walipoteza mechi ya nyumbani baada ya kuchapwa na wageni wao Mathare United Women mabao 3-1 katika mechi iliyochezwa Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Oserian huko Naivasha.

https://t.me/magoti

# Kenya na Tunisia zatwaa ushindi wa Tenisi ya Davis Cup

**NA PAUL WANDERA**

Timu ya Kenya na wenzao kutoka Tunisia ndio washindi wa mchuano wa bara Afrika katika mchezo wa tenisi ya Davis Cup Kundi la tatu ambao ulimalizika katika ugaa wa Nairobi Club siku ya Jumapili.

Kenya ilizishinda timu za Nigeria, Benin na Mozambiki ilihali Tunisia walitwa ushindi baada ya kuwalemea Namibia, Algeria na Madagascar katika mashindano yalioshirikisha mataifa nane.

Sasa Kenya na Tunisia zitapanda daraja na kushindana katika kundi la pili la Davis Cup ya bara Ulaya na Africa (Euro/Africa) mwaka wa 2020.

Kocha wa Kenya Rosemary Owino aliwalimbikizia sifa sufufu wachezaji wa Kenya Ishmael Changawa kutoka Mombasa, Ibrahim Kibet, Kevin Cheruiyot na Albert Njogu.

Ibrahim Kibet, ambaye alimushinda Bruno Nhavene 7-6 (6), 6-4 wa Mozambiki na kuinawirisha ndoto ya Kenya kupanda gazi.

Mwaka Uliopita, Kenya ilikuwa imepata ushindi pamoja na Namibia lakini matumaini yao ya kupandishwa daraja hadi kundi la Pili bara Africa na Ulaya layikatizwa na chama cha mchezo wa tenisi duniani ITF. Hii ni baada ya ITF kutoa msimamo mpya wa mataifa bora ambao uliorodhesha Kenya ya 14 barani Africa.

### Daraja ya pili

Mataifa 12 pekee ndio yaliokubaliwa kushiriki katika michezo ya daraja ya pili. Kenya ililazimika kushiriki tena mashindano ya daraja ya tatu mwaka huu na sasa imetwa ubingwa, pamoja na Tunisia ambao utaiwezesha kushiriki katika mashindano ya Davis Cup daraja ya pili mwaka ujao.

"Matumaini yetu yalikuwa kushinda hapa nyumbani na kupata kupandishwa daraja. Tumeyatimiza hayo yote na sasa jukumu kuu ni kwa hawa vijana kuongeza bidi katika mazoezi yao na kufahamu kuwa mashindano yameboreshwa hasaa katika daraja la pili katika mataifa ya Ulaya na Afrika mwaka wa 2020.

"Kenya ilitwaa ushindi dhidi ya Mozambiki ilihali Tunisia waliwalemea Madagascar katika mechi za fainali," alisema kocha Owino.

Kocha Owino aidha alisema kikosi cha Kenya kitasafiri kwenda Cairo, Misri kwa mashindano mengine ya kujipima nguvu na kumalizia Lagos, Nigeria katika kindumbwendumbwe kingine mnamo Desemba.

Timu ya Kenya ilikuwa imekita kambi mjini Valencia, Uhuspania kujiandaa kwa shindano la Bara Afrika lililokua Rabat, Morocco na Davis Cup iliandaliwa Nairobi.

# Makocha wa soka wahitimu mafunzo ya ukufunzi Mombasa

**NA ANTHONY AROSHEE**

Jumla ya makocha 16 kutoka katika eneo bunge la Likoni walihitimu kozi za msingi za Waalimu wa timu za soka maarufu kama Basic Coaching Course baada ya kumaliza mafunzo ya wiki moja yaliyofanyika kwenye uwanja wa Masoud Mwahima katika Kaunti ya Mombasa.

Mafunzo hayo yaliyofanyika wiki iliyopita, yaliandaliwa na Chama cha Makocha wa Kandanda nchini KEFOCA tawi la Pwani chini ya mwenyekiti wake, Yusuf Harub kwa madhumuni ya kuinua viwango vya ukufunzi na kuboresha viwango vya usakataji kabumbu kuanzia ngazi ya mashinani.

Na pia wakufunzi hao wamepata ufahamu kuhusu wanachohitajika kufunza wanapokuwa mazoezini na wachezaji.

Kozi hiyo iliendeshwa na mwalimu wa Shirikisho la Soka barani Afrika CAF(CAF Instructor) ambaye pia ni kocha wa zamani wa timu ya taifa ya Kenya, Harambee Stars, Mohamed Kheri aliyesaidiana na kocha wa Bandari Youth FC David Lenjo pamoja na beki wa zamani wa Bandari FC Mohamed Kai.

Katika mafunzo hayo, kulikuwa na makocha watatu wanawake Cynthia Mumo wa Ocean Ladies FC kutoka mtaa wa Timbwani, Zainabu "Terry" Atieno wa Vyemani Ladies FC na Zaina Athman wa Young Stars FC, zote kutoka Shikaadabu.

"Makocha hawa ambao wamehitimu sasa wana ujuzi wa kuboresha viwango vya soka kwenye eneo hili(Likoni) na mkoani Pwani kwa ujumla, na mafunzo kama haya KEFOCA imeshaanda sehemu nyingine za hapa Mombasa na mkoani kama vile Kwale na Kilifi," alisema Harub ambaye ni kiungo mshambuliaji wa zamani wa klabu ya Mwenge FC na KTM ya Thika Kaunti ya Kiambu katika miaka ya 80.

Harub aliiambia Pambazuko Michezo kuwa, chama chao cha Makocha KEFOCA imepanga kuandaa kozi nyingine mjini Voi katika Kaunti ya Taita Taveta mapema ya mwezi Desemba mwaka huu.

Makocha wengine waliohitimu ni Bernard Okeyo wa Kishada FC, Juma Mwakuwanga wa Super Eagles FC, Issa Mwamgula wa Young Heroes na Ali Juma wa Piskom FC timu hizo zote kutoka Mtongwe, Bakari Mtsumi wa Change Youth FC, Mohamed Nzallah wa Scud FC na Ali Maboko wa Change Youth FC wote kutoka Shikaadabu.

Wengine ni Joseph Ngumbao wa Ocean Stars FC, Mohamed Kuyeya wa Kitaka FC zote kutoka Timbwani, Kidzao Nyanje wa Likoni Queens, Jumanne Masika wa Likoni Starlets FC, Idd Mwinyikondo wa Likoni Spurs FC na Likoni Secondary Scholl pamoja na Ali Msaada wa Sparki Youth FC kutoka Mvita. KEFOCA ilianza kutoa mafunzo ya ukufunzi kuanzia mapema mwezi Januari, mwaka huu.





**Mwenyekiti wa makocha jimbo la pwani Yusuf Harub akitoa wasia kwa baadhi ya makocha wa mashinani waliohitimu mafunzo yao juzi.** KANDO **Mwenyekiti wa chama cha makocha pwani Yusuf Harub.**

Pambazuko

6 161104 540091

Toleo Nambari 20180198334 | Septemba 18 - 24, 2019 | Gazeti Lako Rasmi | Ksh 40

# EPL: Liverpool yapanua mwanya, City yateleza

NA THABIT POPPATS

Watoto wa Jurgen Klopp, Liverpool wamedhibiti uongozi kileleni hukumahasimu wao Man-City wakitekeleza katika mchakamchaka wa ngoma hii ya ligi kuu ya Uingereza-EPL.

Wakiwa uga wa nyumbani wa Anfield mabingwa hawa wa Ulaya waliwapepeta New Castle 3-1 kupitia kwa Sidio Mane (2) na Mohammed Salah (1).

Man-City waliokuwa unyounyo kama fisi anayesubiri nofu la nyama lidondoke walikula huuwakupoteza alama tatu nyeti kwa kurambishwa na wageni Norwich ugenini 3-2.

Kwa matokeo hayo Liverpool wakokidedea kwa alama 15 baada ya mechi tano huku Man-City wakiwa na alama 10 kwa mechi sambamba.

Nafasi ya tatuinashikiliwa na Tottenham Hotspurs kwa alama nane na Man-U ni ya nnee kwa alama nane.Leicester inakamilisha tano bora kwa alama nane.

Mkiani kuna Watford, Wolves na Aston Villa. Hawa lazima wajitahidi ama EPL wataiona paa kwani wamezembea pakubwa.

Mbali na matokeo ya vinara wa juu ni kuwa Man-U hatimaye walishinda 1-0 dhidi ya Leicester.Brighton walitoka sare 1-1 na Burnley.

Kwengineko Bourmouth walishinda Everton 3-1 huku Southampton ikikosa heshima za mgeni kwa kuwalima wenyeji Sheffield United moja mtungi.

Watford na Arsenal waliagana sare ya 2-2. Hii ni thihirisho tosha kuwa Kocha wa Arsenali Urnai Emery yungali hajaelewa ni safu ipi ya timu yake yahitaji kupigwa jeki. Kocha huyo alimuondoa Mesut Özil na kumuingisha chipukizi Joe Willock.

Kwingineko, mvua ya mabao ilionekana kwani Chelsea iliingia wazimu kwa kuwarambisha mbweha wa Wolves 5-2 kwao.



**Virgil van Dijk na Sadio Mane washerehekea kufunga bao.** RIGHT: **Kocha wa Man City Pep Guardiola.**



Mvua nyingine ni pale Tottenham Hotspurs ilipowatwanga Crystal Palace 4-0. Kwa hali inavyoonekana nikuwa ligi hii ni kali na kila timu inajitahidi kwa udi na uvumba kunawiri.

https://t.me/magazeti

## Bandari hoyee

Bandari FC ilifanya vitu vyake bab kubwa kwa kuwachapa watunisia US Ben Guerdane 2-0 ugani Kasarani katika kinyang'anyiro cha Confederation Cup mkondo wa kwanza.

Mkongomani Yema Mwama aliunganisha kwa kichwa kikali kutoka kwa krosi ya Abdallah Hasaan dakika ya 74 mpaka ndani.

Dakika nne baadaye Hassan alifunga kwa kichwa kutoka kwa krosi ilotoka kwa mganda William Wadri na kuhitimisha ushindi mtamu wa 2-0.

Kwa matokeo hayo Bandari inahitaji sare ya aina yoyote kule Tunisia majuma mawili yajayo kusonga mbele katika hatua ya makundi.

## Utundu na vituko vya Louis Suarez

Louis Suarez ni mmoja ya wachezaji wenye vituko vya hali ya juu.Ni mchezaji wa timu ya taifa ya Uruaguay na klabu maarufu cha Barcelona nchini Uhispania.

Baadhi ya vituko vya Suarez ni pamoja na ufedhuli, kuuma wachezaji wenzake na kupigana uwanjani.Huyu ameshangaza wadau wengi wa soka kwa vituko vya aina yake.

Mnamo mwaka 2011 akiwa mchezaji wa Liverpool alimtusi na kumtukana kwa lugha ya kibaguzi mchezaji mweusi mfaransa wa timu ya Manchester United Patrice Evra.

Kwa ubaguzi huo ambapo alimuita Evra 'nyani ' alipigwa marufuku ya mechi nane na kutozwa pauni elfu 40 za Uingereza.

Mnamo mwaka 2009 akiwa mazoezini katika timu yake ya Ajax Amsterdam kule Uholanzi alipigana na mchezaji mwenzake wa timu hiyo Albert Luque.

Hakukoma hapo kwani kuna kile kisanga kilichotokea katika robo fainali ya kombe la dunia kule Afrika Kusini kati ya taifa lake Uruaguay na Ghana.



Ikiwa imebakia dakika chache mpira kwisha kapteni wa Ghana Asamoah Gyan alichapa mpira uliiokuwa unaingia katika neti kwa ulaini.Hapo Suarez alituka na kuuzuia kwa mkono na kuwa penalti ambayo Gyann alipoteza na Ghana kuwa nje!

Tabia nyingine mbovu ya Suarez ni kuuma wachezaji wenzake kama jitoto jichanga. Ameshawahi kuuma wachezaji watatu uwanjani huku akiwaacha alama ya meno mwilini.



**KInara wa Gor Mahia Kenneth Muguna akisherehekea na mwenzake Boniface Omondi baada ya kufunga bao dhidi ya Tusker.** PICHA: STAFFORD ONDEGO.

## KPL: Sare sufufu zashuhudiwa

NA THABIT POPPATS

Matokeo ya mechi mbali mbali yamedhihiri sare kwa timu karibu zote kukiwa na mabao machache yalotua katika neti wikiendi ilopita.

Tusker FC ilitoka sare 1-1 dhidi ya Mathare United sambamba na Posta Rangers ilipobanana kwa mabao hayo hayo dhidi ya Kakamega Homeboys ugani Machakos.

Kwengineko sare za yai bin yai zilishihudiwa pakubwa ambapo Ulinzi na Sofapaka waliachana hivyo sambamba na ngoma kati ya Western Stima na Wazito FC.

Kavu bin kavu nyingine ilishuhudiwa kati ya wanabenki KCB dhidi ya Kisumu All Stars huku nao AFC Leopards ikilazimishwa sare nyingine na mapapa wa Kariobangi Sharks 0-0.

Gor Mahia na Bandari watacheza dhidi ya Chemelil Sugar na Zoo Kericho mtawalia kesho alhamisi kwani walikuwa kwa mechi za kimataifa wikiendi.

Kimsingi ligi kuu imeashiria makali ya mapema na ni mapema kutowa mwelekeo kwani mambo bado mkoko ndio mwanzo waalika maua wakwetu walinena. Nakubali.